**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Wizara ya Maendeleo ya Mifugo**

# SERA YA TAIFA YA MIFUGO

**DESEMBA 2006**

# YALIYOMO

**DIBAJI** ........ ii
**FAHARASA** ........ v
**VIFUPISHO NA ISTILAHI** ........ viii
**SURA YA KWANZA** ........ - 1 -
**1.0 UTANGULIZI** ........ - 1 -
**1.1 Muhtasari** ........ - 1 -
**1.2 Mafanikio ya Sekta ya Mifugo** ........ - 3 -
**1.3 Vikwazo vinavyokabili Maendeleo ya Sekta ya Mifugo** ........ - 4 -
**1.4 Fursa za Uendelezaji Mifugo** ........ - 5 -
**1.5 Umuhimu wa kuwa na Sera ya Taifa ya Mifugo** ........ - 5 -
**1.6 Mpangilio wa Andiko la Sera** ........ - 6 -
**SURA YA PILI** ........ - 7 -
**2.0 DIRA, DHAMIRA NA MADHUMUNI** ........ - 7 -
**2.1 Dira** ........ - 7 -
**2.2 Dhamira** ........ - 7 -
**2.3 Madhumuni** ........ - 7 -
**SURA YA TATU** ........ - 8 -
**3.0 HOJA, MADHUMUNI NA MATAMKO** ........ - 8 -
**3.1 Nyama** ........ - 8 -
3.1.1 Ng'ombe wa Nyama ........ - 8 -
3.1.2 Kondoo na Mbuzi ........ - 9 -
3.1.3 Kuku ........ - 10 -
3.1.4 Nguruwe ........ - 10 -
3.1.5 Vyanzo Vingine vya Nyama ........ - 11 -
3.1.6 Usindikaji, Masoko na Ulaji wa Nyama ........ - 12 -
**3.2 Maziwa** ........ - 13 -
3.2.1 Ng'ombe wa Maziwa ........ - 13 -
3.2.2 Mbuzi wa Maziwa ........ - 14 -
3.2.3 Nyatimaji na Ngamia ........ - 15 -
3.2.4 Usindikaji, Masoko na Unywaji wa Maziwa ........ - 15 -
**3.3 Ngozi** ........ - 16 -
**3.4 Mazao Mengine ya Ziada Yatokanayo na Mifugo** ........ - 17 -
**3.5 Usimamizi wa Rasilimali za Nyanda za Malisho Katika Maeneo ya ufugaji na ukulima-ufugaji** ........ - 17 -
3.5.1 Matumizi ya Nyanda za Malisho ........ - 17 -
3.5.2 Uzalishaji wa Malisho na Mbegu. ........ - 18 -
3.5.3 Masalia ya Mazao ........ - 19 -
3.5.4 Hifadhi ya Malisho ........ - 19 -
**3.6 Vyakula vya Viwandani** ........ - 21 -
3.6.1 Vyakula Vilivyoongezewa Virutubisho ........ - 21 -
3.6.2 Viungio vya Vyakula vya Mifugo ........ - 22 -
**3.7 Uwiano wa Mifugo na Malisho** ........ - 22 -
**3.8 Wanyama-kazi** ........ - 23 -
3.8.1 Nguvu-kazi ya Wanyama ........ - 23 -
3.8.2 Zana za Mifugo ........ - 24 -
3.8.3 Samadi na Biogesi ........ - 24 -
**3.9 Uendelezaji wa Uzazi wa Mifugo** ........ - 25 -
**3.10 Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo** ........ - 25 -
**3.11 Huduma za Utabibu wa Mifugo** ........ - 26 -

3.11.1 Utoaji wa Huduma za Afya ya Mifugo - 26 -
3.11.2 Magonjwa ya Mlipuko kwa Mifugo - 27 -
3.11.3 Wadudu-ambukizi na Magonjwa Waenezayo - 28 -
3.11.4 Magonjwa Mengine ya Mifugo - 29 -
3.11.5 Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake - 30 -
3.11.6 Mfumo wa Maabara za Mifugo - 30 -
3.11.7 Magonjwa ya Mifugo Yanayoambukiza Binadamu na Usalama wa Vyakula Vitokanavyo na Mifugo. - 31 -
**3.12 Utafiti wa Mifugo - 32 -**
**3.13 Bioteknolojia na Matumizi Salama - 33 -**
**3.14 Kilimo Hai katika Ufugaji - 33 -**
**3.15 Huduma za Ugani - 34 -**
**3.16 Mafunzo ya Mifugo - 35 -**
**3.17 Taarifa na Takwimu za Mifugo - 36 -**
**3.18 Dawa za Tiba na Kinga ya Wanyama - 36 -**
**3.19 Ustawi wa Wanyama - 37 -**
**3.20 Maadili katika Utoaji wa Huduma za Utabibu wa Mifugo - 38 -**
**3.21 Ujuzi Asilia katika Kuendeleza Ufugaji - 38 -**
**3.22 Wanyama Rafiki - 39 -**
**3.23 Masuala ya Kisekta na Mtambuka - 39 -**
3.23.1 Umiliki wa Ardhi kwa Ufugaji - 40 -
3.23.2 Ufugaji Kandokando ya Miji - 40 -
3.23.3 Hifadhi ya Mazingira - 41 -
3.23.4 Masuala ya Jinsia katika Tasnia ya Mifugo - 41 -
3.23.6 Miundombinu - 42 -
3.23.7 Fedha na Mikopo - 43 -
**SURA YA NNE - 44 -**
**4.0 MPANGO NA MFUMO WA UTEKELEZAJI WA SERA - 44 -**
**4.1 Mfumo wa Utekelezaji - 44 -**
**4.2 Mfumo wa Kitaasisi - 44 -**
**4.3 Majukumu ya Wadau - 44 -**
4.3.1 Wizara za Sekta ya Kilimo - 44 -
4.3.2 Sekta ya Umma - 45 -
4.3.3 Sekta Binafsi - 46 -
4.3.4 Washirika katika Maendeleo - 47 -
**4.4 Mfumo wa Uratibu - 47 -**
**SURA YA TANO - 49 -**
**5.0 URATIBU NA USIMAMIZI WA SERA - 49 -**

# DIBAJI

Sekta ya Mifugo ina nafasi kubwa katika kujenga uchumi imara wa Taifa, kuongeza kipato kwa Watanzania wanaotegemea mifugo, na kutoa fursa za ajira sanjari na kuhifadhi rasilimali za Taifa. Sera hii inaeleza nia ya Serikali na wadau wengine katika kukabiliana na changamoto zinazokabili Sekta ya Mifugo.

Jukumu kubwa ni kujenga mazingira mazuri yatakayotoa fursa za kuongeza kipato na ajira kwa wafugaji wadogo, kufuga kibiashara na kuongeza ajira. Ili kufikia haya, malengo makuu matatu ya kisera yatatekelezwa kama ifuatavyo:-

- Kuendeleza Sekta ya Mifugo itakayokuwa na mwelekeo wa kibiashara, yenye ufanisi na itakayohimili ushindani wa kimataifa;
- Kuibua mifumo bora ya uzalishaji itakayoongeza tija miongoni mwa wafugaji wadogo; na
- Kuhifadhi rasilimali za mifugo na kuunda sera na taasisi zitakazosimamia maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

Mabadiliko yanayotarajiwa katika Sekta ya Mifugo ni sehemu ya mchakato mzima wa kuleta maendeleo vijijini ambayo ni pamoja na Programu ya Kuboresha Serikali za Mitaa, umilikishaji wa ardhi kwa wananchi, uwekezaji katika miundombinu na utoaji wa huduma bora za jamii. Marekebisho haya yanalenga kuchangia katika kutekeleza Dira ya Maendeleo Tanzania 2025 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Aidha, mafanikio katika Sekta ya Mifugo, yatategemea ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kupunguza umaskini.

Yapo mabadiliko chanya katika Sekta ya Mifugo nchini ambayo yameanza kujionyesha, hususan katika uzalishaji na uuzaji wa mifugo na mazao yake nje ya nchi, utoaji wa huduma na upatikanaji wa pembejeo za mifugo. Mkazo wa Serikali utaendelea kuwekwa katika kugharamia huduma za ufugaji zinazohitajika kukuza sekta kwa ufanisi. Huduma hizo ni pamoja na miundombinu ya vijijini, utafiti, huduma za ugani, uzuiaji magonjwa ya mlipuko na udhibiti wa wadudu waenezao magonjwa ya mifugo. Aidha, Serikali itahamasisha wafugaji na wadau wengine kuchangia gharama za utoaji wa huduma kama vile ujenzi wa malambo na majosho.

Mashamba makubwa ya mifugo yana uwezo wa kuongeza viwango vya uzalishaji na uuzaji wa mifugo na mazao yake nje ya nchi, ajira na kuboresha maisha ya wafanyakazi wake. Mkakati umetumika wa kugawa mashamba makubwa ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (KARATA) na yale yaliyokuwa chini ya Kampuni ya Ng'ombe wa Maziwa (DAFCO) kuwa mashamba yenye ukubwa wa kati kwa ajili ya ufugaji wa kibiashara unaolenga kutekeleza dhana hii. Mkakati huu umeongeza upeo wa umilikaji mashamba na pia kuwawezesha Watanzania kuingia katika ufugaji wa kibiashara. Maeneo ya ranchi za KARATA yaliyobaki yataendelea kutumika kama ranchi za mfano na maeneo yasiyo na magonjwa ya mifugo kwa ajili ya soko la nje ya nchi.

Kwa muda mrefu ujao, Watanzania walio wengi wataendelea kuishi vijijini. Kaya maskini zilizopo vijijini zitahimizwa kushiriki katika uzalishaji mifugo, hususan kupitia ufugaji wa wanyama kama sungura, simbilisi, ngamia na kanga kwa ajili ya kupunguza umaskini, kuongeza ajira na kuwa na uhakika wa chakula.

Changamoto kubwa inayoikabili tasnia ya mifugo ni namna ya kufikia viwango vya ubora wa mifugo na mazao yake vitakavyokidhi mahitaji ya soko la kikanda na kimataifa. Kwa hiyo, tasnia hii itashiriki kikamilifu katika biashara ya kimataifa kwa kuongeza uuzaji wa mazao nje ya nchi na kukabili ushindani wa bidhaa zinazoingizwa nchini ambapo ulinzi pekee uliopo kwa viwanda vya ndani ni kuweka viwango muafaka vya ushuru na ubora unaotakiwa. Marekebisho ya kisera ya kuifanya biashara ya mifugo iendane na mfumo wa kisasa wa biashara ya kimataifa yamekamilika na Tanzania itajihusisha kikamilifu kuleta mabadiliko zaidi katika mifumo ya biashara hiyo.

Katika nchi za Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, juhudi ya kutekeleza itifaki ya soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) zinaendelea kwa lengo la kuwa na biashara pana inayohusisha mazao ya mifugo ambayo yatachangia ukuaji na maendeleo ya biashara.

Inatia moyo kwamba mabadiliko ya haraka yaliyotokea katika Sekta ya Mifugo katika miaka ya karibuni yamepokelewa na kukubaliwa na wadau wa Sekta wakiwemo wazalishaji, wasindikaji, wafanyabiashara, wauzaji wa pembejeo za mifugo na watoa huduma wengine wapya. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya maeneo ya pembezoni ambayo hayapati huduma za kutosha. Taratibu zitafanywa kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa kuboresha huduma za mifugo katika maeneo haya.

Dira ya Sekta ya Mifugo kama ilivyokubaliwa na wadau wa Sekta mwezi Aprili 2001 inatamka, ***"Kuwe na Sekta ya Mifugo ambayo ifikapo mwaka 2025 kwa sehemu kubwa, itakuwa na ufugaji wa kisasa na endelevu, yenye mifugo bora, yenye uzalishaji mzuri, inayoendeshwa kibiashara na yenye kuboresha lishe ya Mtanzania, kuinua kipato cha mfugaji na Taifa na kuhifadhi mazingira".*** Washiriki katika Sekta ya mifugo wana majukumu ya pamoja ambayo mafanikio yake yatawanufaisha wananchi wote. Hivyo, andiko hili la Sera linatoa mfumo thabiti wa matamko ya sera yatakayowezesha wadau wote kuwa na mwelekeo mmoja wa kuendeleza sekta kwa kujiamini.

Sera hii itakuwa nyenzo muhimu katika kufanikisha Dira ya Sekta ya Mifugo iliyotajwa hapo juu. Malengo ya muda mrefu ni kuwa na uhakika wa chakula, kupunguza umaskini, kuchangia katika uchumi wa nchi na hivyo kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo katika pato la Taifa. Ili madhumuni ya Sera hii yafanikiwe, Wizara itaandaa mikakati na mipango ya utekelezaji wake.

Sera hii ni matokeo ya uwajibikaji wa pamoja na ushirikiano wa wadau mbalimbali walioshiriki kuiandaa. Napenda kuwashukuru wote ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia katika matayarisho ya Sera hii.

Kwa wote nasema, ahsanteni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya.

Anthony Mwandu Diallo (Mb),
Waziri wa Maendeleo ya Mifugo,
**DAR ES SALAAM.**
Desemba, 2006

# FAHARASA

Fasili zilizotumika ni kwa madhumuni ya andiko la Sera ya Taifa ya Mifugo tu. Fasili hizi zinalenga kupunguza tofauti za tafsiri zinazoweza kujitokeza na kuongeza uwazi wa maana ya maneno mbalimbali yalivyotumika katika andiko hili.

| | |
|---|---|
| **Benki ya Jeni** | Ni sehemu maalum ya kuhifadhia kosaafu za wanyama au mimea. Hii inajumuisha wanyama, mimea, viini tete, yai pevu, manii, yai na shangarithishi (DNA). |
| **Bio-anuwai** | Ni aina na mbalimbali za wanyama, mimea na vimelea watumiwao moja kwa moja au kwa njia zinginezo kwa ajili ya uzalishaji wa chakula na mifugo ikiwemo mazao, mifugo, misitu na uvuvi. Vilevile inahusisha viumbe tofauti wasiovunwa ambao wanasaidia katika uzalishaji (kama; vimelea wa ardhini, wanyama wawindao, wachavushaji na wengineo) pamoja na wale walioko katika mazingira kwa ujumla wake wanaosaidia mfumo wa ikolojia ya kilimo (kama; mifugo, nyanda za malisho, misitu na viumbe wa majini), kwa pamoja katika anuai ya mfumo wa ikolojia ya kilimo. |
| **Bioteknolojia** | Ni matumizi ya mfumo wa kibailojia wa kuzalisha zao, na kutumia mfumo wa kibailojia kama zao **AU** matumizi ya mbinu za bioteknolojia kuwezesha kwa njia nyingine kuzalisha zao, kusindika au kutoa huduma. |
| **Huduma za mifugo** | Ni huduma zinazowezesha shughuli zote za uendelezaji wa mifugo, ambazo ni pamoja na mafunzo, utafiti, ugani, huduma za afya ya mifugo, wanyama-kazi, mikopo, uhifadhi, usafirishaji, usindikaji, usambazaji wa pembejeo n.k. |
| **Huduma za Uendelezaji wa nyanda za malisho** | Hujumuisha usimamizi wa malisho, mipango ya malisho, masoko ya mifugo, vitendea kazi, upatikanaji wa maji na malisho, ili kuongeza uzalishaji wa malisho na mifugo yenye tija na endelevu. |
| **Huduma za ugani** | Ni uhawilishiaji wa teknolojia kutoka kwa wataalam kwenda kwa wafugaji. Neno "wataalam" linajumuisha pia wafugaji wenye uwezo wa kutoa huduma hizi kwa wafugaji wengine. |
| **Jeni** | Ni kiini kikuu cha urithi ambacho hubainisha umbile na tabia ya mnyama. |
| **Kilimo** | Shughuli za binadamu zinazohusiana na uzalishaji wa mazao, mifugo, uvuvi na misitu. |
| **Koo ya kigeni** | Ni aina ya mifugo yenye asili ya kigeni. |
| **Koo za asili** | Ni aina ya koo ambayo inastahimili mazingira maalum yenye muundo uliojengeka kwa karne nyingi, kutokana na maendeleo ya kijamii pekee au kikundi chenye utamaduni fulani. |

| | |
|---|---|
| **Kuzaliana kinasaba** | Ni kitendo cha kuzalisha uzao baina ya wazazi wa nasaba moja |
| **Madawa ya Mifugo** | Madawa ya Mifugo hujumuisha dawa za tiba, kemikali, kibiolojia ambazo hutumika katika kutibu, kuzuia na kutambua magonjwa ya wanyama ili kuongeza uzalishaji wenye tija. |
| **Manii/shahawa** | Ni mbegu za kiume na ugiligili unaozalishwa kwenye korodani na aina nyingine za mfumo wa uzazi wa kiume wa mnyama. |
| **Masalia ya mazao** | Ni masalia ya mazao ya shambani baada ya kuvuna yenye lishe kwa ajili ya mifugo |
| **Mchuuzi wa maziwa** | Ni mtu yeyote anayehusika na mauzo ya maziwa au bidhaa zitokanazo na maziwa kwa kupeleka kwenye makazi au kwenye sehemu ya kuuzia. |
| **Mdau** | Ni mtu binafsi, kikundi, asasi au taasisi, sekta binafsi au ya umma ambazo kwa njia moja au nyingine hujishughulisha na uzalishaji na uendelezaji wa mifugo nchini. |
| **Mfugaji** | Ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji. |
| **Mifugo** | Ni wanyama wanaofugwa. |
| **Mkakati** | Ni mbinu inayotumika kufikia madhumuni na malengo yaliyowekwa. |
| **Mnyama** | Ni mnyama yeyote mwenye au asiye na uti wa mgongo isipokuwa binadamu. |
| **Mnyama rafiki** | Ni mnyama mdogo anayefugwa kwenye kaya. |
| **Nyanda za malisho** | Ni eneo kubwa ambalo halilimwi na lina uwezo wa malisho kuhimili mahitaji ya wanyama. |
| **Nyenzo za Sera** | Ni hatua zinazotumika katika kutekeleza Sera kwa mfano, Kodi maalumu, sheria, au kanuni nk |
| **Sera** | Ni mwongozo unaolenga kufikia malengo yaliyokusudiwa. |
| **Serikali** | Ina maana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **Tanzania** | Ina maana ya Tanzania Bara |
| **Tasnia ya maziwa** | Ni sehemu au eneo linalotumika katika kuzalisha na kusindika maziwa au bidhaa zitokanazo na maziwa kwa ajili ya kuuza. |
| **Tasnia ya mifugo** | Hujumuisha shughuli zote zinazohusika na uzalishaji na uendelezaji wa mifugo |
| **Uchungaji wa kuhama (Pastoralism)** | Ni mfumo wa ufugaji ambao mfugaji hutegemea mifugo na mazao yake pekee kukidhi maisha na kujipatia kipato. Aidha, mfumo huu huendana na desturi ya kuhamahama kwa ajili ya kutafuta maji na malisho ya mifugo. |
| **Uendelezaji wa nyanda za malisho** | Inahusu kuendeleza malisho, maji, matumizi na hifadhi ya nyanda za malisho. |
| **Uhamilishaji** | Ni mbinu inayotumika kupata mbegu kutoka kwenye dume, kuihifadhi na kisha kuipandikiza kwa kutumia mrija kwenye kiungo cha uzazi wa mnyama jike aliyepevuka. |

| | |
|---|---|
| **Uhamishaji viinitete** | Ni mbinu inayotumika kuhamisha kiini tete kutoka kwenye jike (mtoaji) na kuingiza kwenye tumbo la uzazi wa jike mwingine (mpokeaji). |
| **Ukulima -Ufugaji** | Ni mfumo wa uzalishaji ambao mzalishaji hutegemea riziki na kipato kutokana na shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. |
| **Uniti za Mifugo (Livestock Units)** | Ni kipimo kilichokubalika kutathmini idadi ya mifugo kwa kuzingatia umri na aina kwa ajili ya uwiano wa malisho na mahitaji ya mifugo au kulinganisha aina tofauti za uzalishaji na aina mbalimbali za mifugo. |
| **Usalamahai (bio-security)** | Ina maana ya kulinda afya za mifugo na binadamu dhidi ya magonjwa. |
| **Uzalishaji chotara** | Kupandisha mifugo kwa kutumia wanyama wenye koo, nasaba au jamii tofauti. |
| **Uzalishaji mayai na Uhawilishiaji viini tete** | Ni matumizi ya mbinu mbalimbali za kuwezesha mnyama jike mtoaji (donor) kutoa mayai mengi kwa wakati mmoja, kupandisha, kutoa viini tete na kuvihamishia kwa mnyama jike mpokeaji (recipient). |
| **Viungio vya vyakula** | (feed additives) |
| **Waziri** | Ni mtu aliyeteuliwa na kupewa dhamana ya kusimamia maendeleo ya mifugo. |
| **Wizara** | Ni Wizara yenye dhamana ya kuendeleza mifugo |
| **Zao la maziwa** | Ni bidhaa iliyotengenezwa kutokana na maziwa kwa kutumia njia zilizokubalika ikiwamo ya kuchemsha, kutenganisha, kuvundika, kuvukiza, kukausha pamoja na maziwa ya mgando, maziwa mala, siagi, jibini, samli, malai, aisikrimu, na bidhaa yoyote inayotengenezwa kwa kutumia maziwa halisi. |
| **Zunosisi (Zoonosis)** | Ni ugonjwa unaoambukiza binadamu kutoka kwa wanyama na kinyume chake. |

# VIFUPISHO NA ISTILAHI

| | | |
|---|---|---|
| AGREST | Agricultural Economics Society of Tanzania | Chama cha Wataalamu wa Uchumi wa Kilimo Tanzania. |
| ASDP | Agricultural Sector Development Programme | Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo |
| ASDS | Agricultural Sector Development Strategy | Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo |
| ASF | African Swine Fever | Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe |
| ASLMs | Agricultural Sector Lead Ministries | Wizara Kiongozi za Sekta ya Kilimo |
| AU/IBAR | African Union Inter African Bureau for Animal Resources | Taasisi ya Raslimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika |
| BSE | Bovine Spongio-form Ecephalopathy | Ugonjwa wa Kichaa cha Ng'ombe |
| CBOs | Community-based Organizations | Asasi za Kijamii |
| CBPP | Contagious Bovine Pleuropneumonia | Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe |
| CCPP | Contagious Caprine Pleuropneumonia | Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi |
| COASCO | Cooperative Audit and Supervision Corporation | Chama cha Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika |
| COSTECH | Commission of Science and Technology | Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia |
| CTI | Confederation of Tanzania Industries | Muungano wa Wenye Viwanda Tanzania |
| CVL | Central Veterinary Laboratory | Maabara Kuu ya Mifugo |
| DAFCO | Dairy Farming Company | Kampuni ya Maziwa Tanzania |
| DNA | Deoxyribo Nucleic Acid | Shangarithishi |
| EAC | East African Community | Jumuiya ya Afrika Mashariki |
| ECF | East Coast Fever | Ndigana Kali |
| FAO | Food and Agriculture Organization | Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa |
| FMD | Foot and Mouth Disease | Ugonjwa wa Miguu na Midomo |
| GDP | Gross Domestic Product | Pato la Taifa |
| IAEA | International Atomic Energy Agency | Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki |
| ITK | Indigenous Technical Knowledge | Ujuzi Asilia katika Kuendeleza Ufugaji |
| KARATA | National Ranching Company | Kampuni ya Ranchi za Taifa |
| LAT | Leather Association of Tanzania | Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania |

| | | |
|---|---|---|
| LEWS | Livestock Early Warning System | Mfumo wa Tahadhari za Majanga kwa Mifugo |
| LFFS | Livestock Farmers Field School | Shamba Darasa la Mifugo |
| LGAs | Local Government Authorities | Serikali za Mitaa |
| LITIs | Livestock Training Institutes | Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo |
| LMUs | Livestock Multiplication Units | Mashamba ya Kuzalisha Mifugo |
| LSD | Lumpy Skins Disease | Ugonjwa wa Mapele Ngozi |
| LU | Livestock Unit | Kipimo cha uwiano wa mifugo na malisho |
| M&E | Monitoring and Evaluation | Ufuatiliaji na Tathmini |
| MAFC | Ministry of Agriculture, Food Security and Cooperatives | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika |
| MDGs | Millennium Development Goals | Malengo ya Maendeleo ya Milenia |
| MKUKUTA | National Strategy for Growth and Reduction of Poverty | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MLD | Ministry of Livestock Development | Wizara ya Maendeleo ya Mifugo |
| MNRT | Ministry of Natural Resources and Tourism | Wizara ya Maliasili na Utalii |
| MOET | Multiple Ovulation and Embryo Transfer | Uhawilishaji wa Viini Tete |
| MWLD | Ministry of Water and Livestock Development | Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo |
| ND | Newcastle Disease | Ugonjwa wa Mdondo wa Kuku |
| NEMC | National Environment Management Council | Baraza la Taifa la Mazingira |
| NEPAD | New Partnership for African Development | Ushirika Mpya wa Maendeleo Afrika |
| NGOs | Non-Governmental Organizations | Asasi zisizo za Kiserikali |
| NIMR | National Institute for Medical Research | Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu |
| OIE | Office Internationale des Epizooties | Shirika la Afya ya Wanyama Ulimwenguni |
| OUT | Open University of Tanzania | Chuo Kikuu Huria cha Tanzania |
| OWM-TAMISEMI | Prime Minister's Office - Regional Administration and Local Government | Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| RDS | Rural Development Strategy | Mkakati wa Maendeleo Vijijini |
| SACAs | Savings and Credit Associations | Ushirika wa Kuweka na Kukopa |
| SACCOs | Savings and Credit Cooperative Societies | Vyama vya Kuweka na Kukopa |

| | | |
|---|---|---|
| SADC | Southern African Development Community | Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika |
| SEGODEN | Southern Eastern Zone Goat Development Network | Mtandao wa Kuendeleza Mbuzi Kanda ya Kusini Mashariki |
| SPS | Sanitary and Phytosanitary | Udhibiti wa Ubora wa Mifugo na Mimea |
| TADs | Trans-boundary Animal Diseases | Magonjwa ya mlipuko yasiyokuwa na mpaka |
| TAFIRI | Tanzania Fisheries Research Institute | Taasisi ya Utafiti wa Samaki (TAFIRI |
| TAFMA | Tanzania Feed Manufacturers Association | Chama cha Usindikaji wa Vyakula vya Mifugo Tanzania |
| TAFORI | Tanzania Forest Research Institute | Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania |
| TAGONET | Tanzania Goat Network | Mtandao wa Kuendeleza Mbuzi Tanzania |
| TAMPA | Tanzania Milk Processors Association | Chama cha Usindikaji wa Maziwa Tanzania |
| TAMPRODA | Tanzania Milk Producers Association | Chama cha Uzalishaji Maziwa Tanzania |
| TANAPA | Tanzania National Parks | Mamlaka ya Hifadhi za Taifa |
| TAWIRI | Tanzania Wildlife Research Institute | Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania |
| TAWLAE | Tanzania Women Leaders in Agriculture and Environment | Chama cha Viongozi Wanawake katika Kilimo na Mazingira Tanzania |
| TBDs | Tick-Borne Diseases | Magonjwa yaenezwayo na Kupe |
| TCAL | Tanzania Chamber of Agriculture and Livestock | Chama cha Wadau wa Kilimo na Mifugo Tanzania |
| TCCIA | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture | Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania |
| TDB | Tanzania Dairy Board | Bodi ya Maziwa Tanzania |
| TDV | Tanzania Development Vision 2025 | Dira ya Maendeleo Tanzania 2025 |
| TFDA | Tanzania Food and Drugs Authority | Mamlaka ya Chakula na Madawa Tanzania |
| TPRI | Tropical Pesticides Research Institute | Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu kwa Nchi za Tropiki. |
| TRA | Tanzania Revenue Authority | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TSAP | Tanzania Society of Animal Production | Chama cha Wataalam wa Uzalishaji Mifugo Tanzania |

| | | |
|---|---|---|
| TSPCA | Tanzania Society for Prevention of Cruelty to Animals | Chama cha Kutetea Haki za Wanyama Tanzania |
| TSZ | Tanzania Shorthorn Zebu | Ng'ombe wa Asili wa Tanganyika |
| TVA | Tanzania Veterinary Association. | Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania |
| VCT | Veterinary Council of Tanzania | Baraza la Veterinari Tanzania |
| VETA | Vocational Education and Training Authority | Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi |
| VICs | Veterinary Investigation Centre | Vituo vya Uchunguzi wa Magonjwa ya Wanyama |
| VPH | Veterinary Public Health | Usalama wa Afya ya Jamii |
| WHO | World Health Organization | Shirika la Afya Duniani |
| WTO | World Trade Organization | Shirika la Biashara Duniani |
| MVIWATA | National Network of Farmers Organisation in Tanzania | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| ASARECA | Association for Strengthening Agricultural Research in Eastern and Central Africa | Asasi ya Kuimarisha Utafiti wa Kilimo katika Nchi za Mashariki na Kati mwa Afrika |
| IFAD | Nternational Fund for Agricultural Development | Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo |
| WB | World Bank | Benki ya Dunia |
| ADB | African Development Bank | Kilimo, Benki ya Maendeleo ya Afrika, |
| JICA | Japan International Cooperation Agency | Shirika la Kimaendeleo la Japani |
| SDC | Swiss Agency for Development and Cooperation | |
| USAID | United State Agency for International Development | Shirika la Misaada la Marekani |
| DFID | Department for International Development | Idara ya Maendeleo ya Uingereza |
| CFC | Common Fund for Commodities | Mfuko wa Pamoja wa Vida |
| DANIDA | Danish International Development Agency | Shirika la Maendeleo ya Denmark |
| NORAD | Norway Agency for Development Cooperation | Shirika la Maendeleo ya Norway |
| BADEA | Arab Bank for Economic Development in Africa | Benki ya Nchi za Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi katika Afrika |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Muhtasari

Tanzania ina rasilimali kubwa ya maliasili ikiwemo ardhi, malisho na idadi kubwa ya mifugo. Kati ya jumla ya hekta milioni 94 za rasilimali ya ardhi, hekta milioni 60 ni nyanda za malisho zinazofaa kwa ufugaji. Kwa sasa kuna ng'ombe milioni 18.5, mbuzi milioni 13.1 na kondoo milioni 3.6. Mifugo mingine inayofugwa nchini ni pamoja na nguruwe milioni 1.2, kuku wa asili milioni 30 (MWLD, Statistical Year Book, 2005). Tanzania ni nchi ya tatu barani Afrika kwa wingi wa ng'ombe baada ya Ethiopia na Sudan. Zaidi ya asilimia 90 ya idadi ya mifugo iliyopo nchini ni ya asili ambayo ukosaafu wake ni mdogo. Wanyama hawa hata hivyo wamezoea mazingira magumu na wanastahimili magonjwa.

Uzalishaji wa mifugo umegawanyika katika mifumo mikuu miwili ambayo ni ufugaji huria na ufugaji shadidi. Mfumo wa ufugaji shadidi japo sio mkubwa nchini, unatiliwa mkazo zaidi katika kuendeleza ufugaji na uwekezaji kwani unachangia zaidi kwenye uchumi wa soko. Kwa upande mwingine, mfumo wa ufugaji huria ambao hufanywa na wakulima wachungaji na wachungaji wahamaji, ni mfumo unaotegemea upatikanaji wa malisho na maji kwa msimu na matokeo yake husababisha wafugaji kuhamahama. Mfumo huu unakabiliwa na matatizo ya utunzaji duni wa mifugo, matumizi duni ya teknolojia za kisasa, kuhodhi mifugo mingi zaidi ya uwezo wa ardhi na ukosefu wa mazingira mazuri ya masoko. Pamoja na matatizo yanayoukabili mfumo huu, bado umeendelea kwa miongo mingi kuwa tegemeo kwa jamii ya wafugaji wahamaji. Ili kuendeleza na kufikia malengo yake, sekta ya mifugo inahitaji sera ya mifugo iliyo pana itakayotoa mwongozo kwa wadau wote.

Kuanzia miaka ya 1980, uchumi wa Tanzania umepitia mabadiliko mbalimbali na muhimu katika kuelekea kwenye uchumi wa soko. Maboresho yaliyofanyika katika sera za uchumi wa kijumla yamesababisha kuwepo kwa tafsiri mpya juu ya majukumu ya sekta ya umma na sekta binafsi katika shughuli za maendeleo ya mifugo. Kutokana na mabadiliko haya Serikali imejiondoa katika shughuli za uzalishaji, usindikaji na masoko, ambazo zinaweza kufanywa vizuri zaidi na sekta binafsi.

Sera hii ni ya tatu kutungwa kuhusu tasnia ya mifugo. Sera ya kwanza ilitungwa mwaka 1983 ikiwa na madhumuni ya kuleta changamoto kwenye maendeleo ya mifugo katika uchumi wa dola. Aidha, Sera hiyo ilitilia mkazo uendelezaji wa mashamba makubwa ya mashirika ya umma kwa ajili ya uzalishaji, usindikaji na masoko.

Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997, ilikuwa sera ya pili kutayarishwa na ilikuwa sanjari na mabadiliko yanayoendelea na iliainisha majukumu ya umma na sekta binafsi. Hata hivyo, wakati wa utekelezaji wa sera hiyo maboresho mengine yalijitokeza na hivyo kuhitajika kuipitia na kuandaa sera hii mpya. Sera mpya ya mifugo itaangalia na kushughulikia masuala muhimu yakiwemo utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake, ustawi wa wanyama, elimu ya asili, usalama na teknolojia ya viumbe hai, ufugaji wa kilimo hai, usalama wa chakula, kuzuka kwa magonjwa mapya ya mifugo, taasisi za kudhibiti mazao ya mifugo na maadili ya wataalamu, hifadhi ya kosaafu za wanyama, ujazo wa wanyama, mfumo wa maabara ya mifugo, majanga yahusuyo mifugo na wanyama rafiki.

Sera hii inalenga kuchochea maendeleo ya tasnia ya mifugo ili iweze kumwongezea kipato mwananchi na Taifa kwa ujumla, kuboresha uhakika wa chakula na hifadhi ya mazingira. Aidha, sera hii imedhamiria kuongeza ubora wa maisha kwa wadau wote wanaojihusisha na sekta ya mifugo nchini.

Utayarishaji wa Sera hii umezingatia mambo yafuatayo:-

(i) Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025;
(ii) Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) 2004;
(iii) Malengo ya Milenia (MDGs);
(iv) Mkakati wa Maendeleo Vijijini (RDS) 2001;
(v) Sera ya Maendeleo Vijijini 2003;
(vi) Sera ya Taifa ya Biashara 2003;
(vii) Maazimio ya Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Mifugo 2001;
(viii) Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS) 2001;
(ix) Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP) 2003;
(x) Waraka wa Rais Namba 1 wa Mwaka 2002;
(xi) Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2004;
(xii) Sera ya Uwekezaji;
(xiii) Sera ya Ardhi1995;
(xiv) Sera ya Taifa ya Mazingira 1997;
(xv) Sera ya Kilimo na Mifugo 1997;
(xvi) Jitihada na Mipango ya Kimataifa na Kikanda
    - Mkataba wa Shirika la Biashara Duniani kuhusu ubora na udhibiti wa mifugo na mazao ya kilimo (SPS).
    - Shirika la Afya Duniani/Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa kuhusu kanuni za ubora na usalama wa chakula (WHO/FAO's Codex Alimentarius).
    - Mpango Mahususi wa Afrika wa Kuendeleza Kilimo (Comprehensive Africa Agriculture Development Programme) wa NEPAD. .
    - Mpango Mkakati Ashiria wa Maendeleo wa Nchi za Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC's Regional Indicative Strategic Development Plan -RISDP).
    - Sera ya Kilimo na Maendeleo Vijijini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki .

## 1.2 Mafanikio ya Sekta ya Mifugo

Sekta ya Mifugo imekuwa na ukuaji wa zaidi ya asilimia 2.7 katika kipindi cha muongo uliopita. Ukuaji huu ni chini ya ukuaji wa idadi ya watu ambao ni asilimia 2.9. Kulingana na MKUKUTA, Sekta ya Mifugo inatarajiwa kukua kwa asilimia 9 ifikapo 2010.

Katika mwaka 2005, mchango wa Sekta ya Kilimo kwenye pato la Taifa ulikuwa ni asilimia 45.6 (Hali ya Uchumi wa Taifa, 2005), ambapo mazao yalichangia asilimia 34.0, mifugo 5.9, uvuvi 3.0, misitu na uwindaji 2.7.,Mchango wa mifugo ulitokana na nyama asilimia 40, maziwa asilimia 30 na kuku na wanyama wadogo asilimia 30. Katika kipindi hicho, Sekta ya Kilimo ilikua kwa asilimia 5.2 ambapo sekta ndogo ya mazao ilikua kwa asilimia 5.2, mifugo asilimia 4.2, uvuvi asilimia 7.3 na misitu na uwindaji asilimia 4.5. Aidha, Sekta ya Mifugo hutoa mazao mengi ya mifugo yanayotumika nchini na hivyo kupunguza uagizaji wa mazao hayo kutoka nje ya nchi. Pamoja na mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye uchumi wa Taifa, pia huchangia katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kuzalisha chakula, hivyo kuchangia katika uhakika wa chakula;
(ii) Kubadilisha malisho na masalio ya mazao kuwa chakula;
(iii) Mifugo ni benki hai kwa wafugaji;
(iv) Chanzo cha mapato na ajira kwa wananchi vijijini;
(v) Kutoa ngozi na mazao mengine;
(vi) Kutoa mbolea na wanyama kazi kwa ajili ya kilimo endelevu;
(vii) Kuchangia katika majukumu ya kijadi kwenye jamii.

Takriban asilimia 40 ya kaya milioni 3.9 za kilimo nchini hujihusisha na uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Upo uwezekano wa kuongeza uzalishaji wa mifugo na tija na kuchangia kwenye pato la Taifa kwa vile uwezo wa ardhi uliopo unaoweza kuhimili hadi uniti za mifugo milioni 20 haujatumika kikamilifu.

Uzalishaji wa nyama kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita (1995 – 2005) uliongezeka kutoka tani 244,000 hadi tani 378,500 sawa na ongezeko la asilimia 55 ambapo sehemu kubwa ilitokana na ufugaji wa asili. Pia, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 555 hadi bilioni 1.38 ambapo asilimia 70 ilichangiwa na sekta ya ufugaji wa asili. Vilevile, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai milioni 380 hadi bilioni 1.8. Katika kipindi hicho, ulaji wa nyama kwa mtu kwa mwaka uliongezeka kutoka kilo 5 hadi 11, unywaji wa maziwa kutoka lita 20 hadi 39 na ulaji wa mayai kutoka 14 hadi 53. Aidha, ukusanyaji wa ngozi uliongezeka kutoka vipande milioni 1.3 hadi milioni 4.0 ambapo kati ya vipande hivyo, asilimia 86 viliuzwa nchi za nje.

Licha ya ongezeko la uzalishaji huo, utekelezaji katika tasnia ya mifugo bado hauridhishi. Hii inatokana na ukuaji hafifu wa mifugo, vifo vingi, uzalishaji duni na mazao yasiyokuwa na ubora unaotakiwa. Uboreshaji wa viwango vya uzalishaji

pamoja na uongezaji wa thamani kupitia usindikaji utaongeza kwa kiasi kikubwa thamani ya mazao na kipato kutokana na tasnia ya mifugo.

## 1.3 Vikwazo vinavyokabili Maendeleo ya Sekta ya Mifugo

Mkutano wa wadau wa tasnia ya mifugo uliofanyika Arusha mwaka 2001, ulibainisha matatizo makuu sita yanayoathiri ufanisi wa Sekta ya Mifugo hapa nchini. Matatizo hayo ni:-

### (i) Ardhi, Maji na Malisho

Tatizo kubwa katika mfumo wa umilikaji wa ardhi, rasilimali za maji na malisho ni kutokuwa na utaratibu wa kutenga na kumilikisha ardhi kulingana na taratibu za kisheria au kimila. Matatizo mengine ni kupanuka kwa shughuli za kilimo katika maeneo yaliyokuwa yanatumika kwa kufuga na kuchungia, kupanuliwa kwa mbuga za wanyamapori na kuhamahama kwa wafugaji kunakozuia kuendelezwa kwa maeneo yao.

### (ii) Aina ya mifugo na mifumo ya uzalishaji

Kuwepo kwa kosaafu duni za mifugo ya asili pamoja na upungufu wa mifugo chotara, kumechangia kwa kiwango kikubwa uzalishaji duni na usio na tija. Hali hii imechochewa kwa kiwango kikubwa na mifumo ya uzalishaji mifugo inayotumiwa na wafugaji. Hata hivyo, mifugo ya asili ina uwezo wa kustahimili mazingira magumu.

### (iii) Magonjwa ya Mifugo

Magonjwa ya mifugo ni kati ya matatizo yanayokabili maendeleo ya tasnia ya mifugo. Kumekuwepo na kuenea kwa magonjwa ya mifugo nchini kama vile magonjwa ya mlipuko yasiyokuwa na mipaka, magonjwa yanayoenezwa na wadudu, magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu na magonjwa yanayojitokeza ambayo ni changamoto kubwa kwa maendeleo ya tasnia ya mifugo.

### (iv) Usindikaji na masoko ya mazao ya mifugo

Upo upungufu wa miundombinu kwa ajili ya usindikaji na masoko ya mifugo na mazao yake. Pia, kumekuwepo na uingizaji wa mazao ya mifugo yenye ruzuku kubwa kutoka nje ya nchi ambayo hukatisha tamaa wawekezaji pamoja na kuleta ushindani usio sawa kwa mazao ya mifugo yanayozalishwa au kusindikwa hapa nchini.

### (v) Elimu na ujuzi kwa wafugaji

Ukosefu wa elimu na ujuzi wa kutosha kwa wafugaji huathiri maendeleo ya tasnia ya mifugo nchini. Elimu na ujuzi ni muhimu na husaidia katika kupokea teknolojia sahihi zinazobuniwa na kusambazwa kwa wafugaji.

### (vi) Uwekezaji na Mikopo

Uhaba wa taasisi za kutoa mikopo kwa wajasiriamali wakubwa, wa kati na wadogo wa mifugo na uwekezaji mdogo vinakwaza upanuzi na uzalishaji wa mifugo kibiashara.

## 1.4 Fursa za Uendelezaji Mifugo

Zipo fursa nyingi zinazoweza kuongeza mchango wa mifugo katika uchumi wa Taifa na uhakika wa chakula katika kaya iwapo fursa hizo zitatumiwa ipasavyo. Fursa hizo ni pamoja na kuwepo kwa:

(i) Idadi kubwa na aina mbalimbali za mifugo;
(ii) Rasilimali kubwa ya ardhi ya malisho ambayo inakadiriwa kuwa hekta milioni 60;
(iii) Hali nzuri ya hewa inayofaa kwa ufugaji katika kanda mbalimbali;
(iv) Masoko ya uhakika ya ndani na nje ya nchi;
(v) Upatikanaji wa watu wa watakaoweza kufunzwa, pamoja na gharama nafuu za utendaji kazi;
(vi) Ujuzi na elimu ya asili kuhusu mifugo;
(vii) Sera nzuri za kiuchumi.

## 1.5 Umuhimu wa kuwa na Sera ya Taifa ya Mifugo

Umuhimu wa kuwa na Sera ya Taifa ya Mifugo nchini ni kuchochea ufugaji wa kibiashara unaolenga kuhifadhi mazingira. Nia ni kuboresha maisha ya wafugaji kwa kuwaongezea kipato na uhakika wa chakula kutokana na mazao ya mifugo; hivyo, kuchangia katika kufikia malengo ya MKUKUTA.

Sera hii imezingatia kuwepo kwa mifugo mingi ikilinganishwa na nchi nyingi za Afrika. Pia, Sera imezingatia hali ya maendeleo yanayotokea wakati huu wa soko huru, utandawazi, ubinafsishaji na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ambavyo vina mchango wa moja kwa moja katika maendeleo ya sekta ya mifugo. Vilevile, sera hii inasisitiza umuhimu wa kuongeza thamani kwa mazao yatokanayo na mifugo ili yaweze kuingia katika soko la ushindani na, pia, kuyaongezea muda wa hifadhi. Aidha, idadi ya watu Tanzania inatarajia kuongezeka na kufikia milioni 55.2 ifikapo mwaka 2025, hali itakayofanya mahitaji ya mifugo na mazao yake kuongezeka na hivyo, kuhitaji juhudi za makusudi za kuongeza tija katika uzalishaji wa mifugo.

Baadhi ya hoja kuhusu Sekta ya Mifugo zilizoainishwa katika Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997 hazikufafanuliwa vya kutosha. Wakati wa utekelezaji wa sera hiyo yalijitokeza mabadiliko mbalimbali ya sera za kiuchumi pamoja na maboresho ya kisekta yaliyosababisha sera hiyo kurejewa na kuandaa sera mpya. Sera hii inalenga kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika sera iliyopita hususan katika maeneo ya udhibiti, utaalam na huduma zitolewazo na sekta mtambuka.

Pia, sera hii inalenga kuangalia masuala muhimu katika Sekta ya Mifugo ambayo hayakuzingatiwa katika sera iliyopita. Masuala hayo ni pamoja na utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake, ustawi wa wanyama, elimu asilia, usalama na teknolojia kwa viumbe hai, ufugaji wa kilimo hai, usalama wa chakula, magonjwa mapya ya mifugo, bodi za udhibiti wa mazao ya mifugo, taasisi za udhibiti wa taaluma, uhifadhi wa kosaafu za wanyama, kufuga kulingana na maeneo ya malisho, mfumo wa maabara ya mifugo, majanga ya mifugo na wanyama rafiki.

Sekta ya Kilimo kwa ujumla wake inajumuisha, kilimo cha mazao, mifugo, uvuvi na misitu. Sekta ndogo za misitu na uvuvi zinazo sera zinazojitegemea; hivyo kutoa umuhimu kuwa na sera zinazojitegemea kwa sekta ndogo za mazao na mifugo.

## 1.6 Mpangilio wa Andiko la Sera

Andiko hili la Sera lina sura tano: Sura ya Kwanza ni Utangulizi; Sura ya Pili inaelezea Dira, Dhamira na Madhumuni; Sura ya Tatu inaelezea kwa undani Hoja, Madhumuni na Tamko la Sera; Sura ya Nne inaelezea Muundo wa Kisheria na Mpangilio wa Kitaasisi na Sura ya Tano inaelezea Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Sera.

# SURA YA PILI

## 2.0 DIRA, DHAMIRA NA MADHUMUNI

### 2.1 Dira

Sekta ya Mifugo inayo dira ya maendeleo inayoendana na Dira ya Maendeleo Tanzania kufikia mwaka 2025, na inatamka kuwa:

***"Kuwe na Sekta ya Mifugo ambayo ifikapo mwaka 2025 kwa sehemu kubwa, itakuwa na ufugaji wa kisasa na endelevu, yenye mifugo bora, yenye uzalishaji mzuri, inayoendeshwa kibiashara na yenye kuboresha lishe ya Mtanzania, kuinua kipato cha mfugaji na Taifa na kuhifadhi mazingira"***

### 2.2 Dhamira

Dhamira ya sekta ya mifugo ni:-
***"Kuhakikisha kuwa rasilimali ya mifugo inaendelezwa na kutunzwa katika mazingira endelevu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi"***

### 2.3 Madhumuni

Madhumuni makuu ya Sera ya Taifa ya Mifugo ni kujenga sekta yenye ufanisi na ushindani ambayo itachangia kuboresha hali ya wananchi, ambao shughuli zao kubwa na maisha hutegemea mifugo.

Madhumuni mahususi ya Sera ya Taifa ya Mifugo ni:-
(i) Kuchangia uhakika wa chakula kitaifa kwa kuongeza uzalishaji, usindikaji na masoko ya mazao ya mifugo ili kukidhi mahitaji ya lishe.
(ii) Kuinua hali ya maisha ya wananchi wanaojihusisha na ufugaji kupitia ongezeko la kipato kutokana na mifugo.
(iii) Kuongeza wingi na ubora wa mifugo na mazao yake kama malighafi kwa ajili ya matumizi ya viwanda vya ndani na nje.
(iv) Kuhimiza matumizi na usimamizi jumuishi na endelevu wa rasilimali zinazohusiana na uzalishaji wa mifugo ili kujenga mazingira endelevu.
(v) Kuimarisha utoaji wa huduma za kiufundi pamoja na kutayarisha na kusambaza teknolojia mpya.
(vi) Kuendeleza rasilimali watu wakiwemo wafugaji.
(vii) Kuhimiza uzalishaji wa bidhaa za mifugo zilizo salama na bora ili kulinda afya za walaji.
(viii) Kuhimiza matumizi ya wanyama-kazi na biogesi
(ix) Kuhusisha masuala ya mtambuka na sekta-mtambuka kama vile jinsia, Virusi vya Ukimwi (VVU)/UKIMWI, ardhi na mazingira.

# SURA YA TATU

## 3.0 HOJA, MADHUMUNI NA MATAMKO

Mifugo hutoa aina mbalimbali za mazao ikiwa ni pamoja na nyama, maziwa, mayai na ngozi. Sura hii inafafanua hoja, madhumuni na matamko ya sera kuhusu mambo yafuatayo:

### 3.1 Nyama

Vyanzo vikuu vya nyama nchini ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku, nguruwe, samaki, wanyamapori na wanyama wengine wanaoliwa. Takribani, asilimia 53 ya nyama inayozalishwa nchini hutokana na ng'ombe na sehemu kubwa ya nyama hiyo hutumika kwa ajili ya soko la ndani na kiasi kidogo huuzwa nje ya nchi.

#### 3.1.1 Ng'ombe wa Nyama

Ng'ombe wa asili aina ya Zebu (TSZ) na Ankole ni chanzo kikuu cha nyama ya ng'ombe hapa nchini. Kuna aina mbalimbali za TSZ kama vile Iringa-Red, Tarime, Maasai, Sukuma, Singida-White na Fipa. Kati ya ng'ombe hawa asilimia 80 wanafugwa katika mfumo wa kilimo-ufugaji na asilimia 14 katika mfumo wa uchungaji wa kuhamahama. Aidha, asilimia sita iliyobaki hufugwa kwenye ranchi na mashamba ya ng'ombe wa maziwa. Asilimia kubwa ya ng'ombe hawa pamoja na chotara wao ni aina ya *Mpwapwa, Boran*, *Charolais, Chianina, Simmental, Hereford, Brahman, Santa Getrudes na Aberdeen Angus.*

**Hoja**

Kwa sasa, uzalishaji wa nyama unakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosaafu duni wa mifugo ya asili iliyopo, miundombinu na masoko hafifu, kuwepo na kuenea kwa magonjwa ya mifugo, uhaba wa vyakula vya mifugo, vyama dhaifu vya wafugaji na uhaba wa huduma za kitaalam.

**Madhumuni**

Kuongeza uzalishaji wa nyama bora inayokidhi viwango vya soko la ndani na nje ili kuongeza kipato cha wafugaji na hatimaye kuboresha hali zao za maisha.

**Tamko la Sera**

(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza uzalishaji wa nyama bora kibiashara katika mfumo wa shadidi na ufugaji wa maeneo makubwa (Ranchi, uchungaji wa kuhama na kilimo-ufugaji) ikiwa ni pamoja na kuimarisha KARATA.

(ii) Serikali itahimiza uorodheshaji, uchambuzi, tathmini na uchaguzi wa koo bora za ng'ombe wa asili kwa ajili ya nyama.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza uboreshaji wa kosaafu kwenye ng'ombe wa asili ili kuongeza tija.

(iv) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa nyama.
(v) Serikali itahamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wafugaji na wafanyabiashara wa ng'ombe wa nyama.
(vi) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaanzisha mfumo wa kutambua, kusajili, na kufuatilia mifugo na mazao yake kwa ajili ya uzalishaji wa nyama bora na salama kwa kuzingatia kanuni bora za uzalishaji.

### 3.1.2 Kondoo na Mbuzi

Ufugaji wa kondoo na mbuzi ni shughuli muhimu ya kiuchumi inayohusisha takribani asilimia 30 ya kaya za wakulima wote na huchangia karibu asilimia 22 ya mahitaji ya nyama nchini. Kondoo na mbuzi wanaofugwa hapa nchini ni wa koo za˵Red-Maasai˝ na Gogo kwa upande wa kondoo; na Ujiji, Newala, Sukuma na Gogo kwa mbuzi. Kondoo aina ya˵Black Head Persian (BHP)˝ na mbuzi aina ya ˵Boer˝ ni koo pekee zilizoingizwa nchini kutoka nje.

**Hoja**
Kondoo na mbuzi hufugwa katika maeneo mengi kutokana na uwezo wao wa kuweza kuishi katika kanda tofauti za ikolojia za kilimo. Kutokana na uwezo wao wa kuzaa mara mbili kwa mwaka, kukua haraka na gharama ndogo za uzalishaji ikilinganishwa na ng'ombe, ufugaji wao unapendwa na wafugaji wadogo. Hata hivyo, uzalishaji wa kondoo na mbuzi bado unakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na lishe duni, magonjwa, kosaafu duni na miundombinu hafifu ya masoko.

**Madhumuni**
Kuhamasisha uzalishaji wa kibiashara na endelevu wa kondoo na mbuzi ili kukidhi soko la ndani na nje na hivyo kuongeza uhakika wa chakula na kipato.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kuongeza uzalishaji wa kondoo na mbuzi.
(ii) Serikali itahimiza uorodheshaji, uchambuzi, tathmini na uchaguzi wa koo bora za kondoo na mbuzi wa asili kwa ajili ya nyama.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza uboreshaji kosaafu kwenye kondoo na mbuzi wa asili ili kuongeza tija.
(iv) Jitihada zitafanywa kuhimiza ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi katika kuboresha na kusimamia mifumo ya masoko.
(v) Serikali itahamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wafugaji na wafanyabiashara wa kondoo na mbuzi.

### 3.1.3 Kuku

Uzalishaji wa kuku nchini umegawanyika katika mifumo ya ufugaji wa asili na kibiashara. Mfumo wa ufugaji wa asili huchangia zaidi ya asilimia 70 ya kuku wote wanaofugwa na hutoa nyama na mayai yanayoliwa vijijini na hukidhi asilimia 20 ya mahitaji ya mijini. Aina kuu za koo na chotara wa kuku wa asili ni *Kuchi, Kishingo, Sukuma, Kinyafuzi* na *Kiduchu*.

Kwa kiwango kikubwa, uzalishaji wa kuku wa kibiashara hufanywa katika maeneo ya mijini na maeneo yanayozunguka miji. Koo za kuku (pamoja na chotara wao) wanaofugwa kibiashara ni pamoja na *White Leghorns, Rhode Island Red, Light Sussex, Plymouth Rock, Hisex, Hybro* na *Shavers*.

**Hoja**

Ufugaji wa kuku wa asili na wa kibiashara unakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, lishe duni, uhaba wa huduma za kitaalam, kosaafu duni na vyama dhaifu vya wafugaji. Vilevile, kuna udhibiti hafifu kwenye vituo vya kutotolea vifaranga na mashamba ya kuku wazazi.

**Madhumuni**

Kuongeza idadi na ubora wa kuku na mazao yake ili kukidhi mahitaji ya ndani, kuongeza mauzo ya nje na kuhamasisha uzalishaji endelevu wa kuku.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam na matumizi ya teknolojia sahihi katika kuongeza uzalishaji wa kuku.
(ii) Serikali itahimiza uorodheshaji, uchambuzi, tathmini na uchaguzi wa koo bora za kuku wa asili kwa ajili ya mayai na nyama.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza uboreshaji kosaafu kwenye kuku wa asili ili kuongeza tija.
(iv) Jitihada zitafanywa kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji, usindikaji na masoko ya kuku na mazao yake.
(v) Serikali itahimiza uanzishwaji wa mashamba bora ya kuku wazazi na vituo vya kutotolea vifaranga.
(vi) Serikali itahamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wafugaji na wafanyabiashara wa kuku.

### 3.1.4 Nguruwe

Ufugaji wa nguruwe umeanza kuenea katika sehemu nyingi hapa nchini na kutoa mchango katika mahitaji ya nyama. Nguruwe wana sifa ya kuzaa watoto wengi, kukua haraka, kutumia chakula vizuri mwilini, kutumia muda mfupi toka kizazi kimoja hadi kingine na huhitaji eneo dogo la kufugia. Licha ya uzalishaji wa nyama, nguruwe pia hutoa mafuta ya kupikia na samadi kwa ajili ya kurutubisha ardhi.

Nguruwe wengi hufugwa na wafugaji wadogo katika mfumo wa kilimo mseto ambapo hutegemea malisho na vyakula vya nyongeza inapobidi. Ufugaji wa nguruwe katika mfumo huu ni duni na hivyo husababisha nguruwe kuzaa vitoto vichache vyenye uzito mdogo katika mzao mmoja, kuwa na maumbile madogo, idadi kubwa ya vifo vya vitoto na ukuaji mdogo.

**Hoja**

Uzalishaji wa nguruwe kibiashara hufanywa na wafugaji wachache wenye kipato cha kawaida wenye uwezo wa kugharamia vyakula na mahitaji mengine ya ufugaji huo. Kuzaliana kwa nguruwe wa ukoo mmoja kunakosababishwa na kukosekana kwa kumbukumbu za uzalishaji ni tatizo katika nguruwe waliopo. Pia, upungufu wa huduma za kitaalam, ukosefu wa machinjio za nguruwe na miundombinu ya masoko, magonjwa, baadhi ya mila na imani za dini kuzuia kula nyama ya nguruwe kumeathiri maendeleo ya uzalishaji nguruwe nchini.

**Madhumuni**

Kuhimiza uzalishaji wa nguruwe ili kuchangia katika uhakika wa chakula, kuboresha lishe, kuongeza kipato na kuhifadhi mazingira.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaaalam na matumizi ya teknolojia sahihi katika kuongeza uzalishaji wa nguruwe.

(ii) Serikali itahamasisha uzalishaji wa vyakula bora vya nguruwe na kuhimiza matumizi ya malighafi na viungio vya vyakula vinavyopatikana hapa nchini.

(iii) Serikali itahimiza uorodheshaji, uchambuzi, tathmini na uchaguzi wa koo bora za nguruwe kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija.

(iv) Serikali itahimiza na kuhamasisha ujenzi wa machinjio zenye ubora na miundombinu ya masoko kwenye maeneo yenye wafugaji na walaji wengi wa nyama ya nguruwe.

(v) Serikali itahamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wafugaji na wafanyabiashara wa nguruwe.

### 3.1.5 Vyanzo Vingine vya Nyama

Tanzania ina aina nyingi za wanyama lakini ni wachache wanaotumika kwa nyama. Vyanzo vingine vya nyama ambavyo matumizi yake hayajazoeleka kwa wengi ni pamoja na sungura na jamii za bata. Hali hii inatoa fursa ya kuzalisha aina nyingi za nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje.

**Hoja**

Wengi wa wanyama hawa hupatikana vijijini. Aidha, uzalishaji na ulaji wake uko chini kutokana na mila na desturi pamoja na uelewa mdogo wa kuendeleza na kudumisha rasilimali hiyo. Vikwazo vingine ni upungufu katika utafiti, ugani na usambazaji wa taarifa kuhusu wanyama hawa.

**Madhumuni**
Kuhamasisha uzalishaji na ulaji wa nyama ya aina hii ili kuongeza uhakika wa chakula katika kaya, kipato na kuboresha lishe.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itahimiza uorodheshaji, uchambuzi, tathmini na uchaguzi wa koo bora za wanyama wa aina hii kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija.
(ii) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kuongeza uzalishaji wa wanyama hawa.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza matumizi na kuboresha uzalishaji, usindikaji na masoko ya wanyama hawa.
(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaandaa na kuhamasisha mfumo endelevu wa kuzalisha wanyama hawa.

### 3.1.6 Usindikaji, Masoko na Ulaji wa Nyama

Hapa nchini kuna zaidi ya minada 300 ya awali, 13 ya upili na sita ya mipakani. Minada yote ya awali inasimamiwa na Halmashauri za Wilaya ambapo minada ya upili na ya mipakani inasimamiwa na Wizara. Minada michache ya awali inafanya kazi ila mingi ni mibovu. Aidha, vipo viwanda sita vya kusindika nyama na machinjio za kisasa saba. Kwa sasa, ulaji wa nyama kwa mtu kwa mwaka ni kilo 11 kiasi ambacho ni chini ya kiwango cha kilo 50 kinachopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO).

**Hoja**
Usindikaji, uuzaji na ulaji wa nyama bora na mazao yatokanayo na nyama unakabiliwa na kutopatikana kwa wanyama bora, uhaba wa taarifa za masoko, upungufu wa utafiti na mafunzo katika teknolojia ya nyama, uelewa mdogo wa walaji kuhusu ubora wa nyama na ukosefu wa mitaji ya kuwekeza katika viwanda vya kusindika nyama. Kutokana na hali hii, baadhi ya kampuni za biashara huagiza nyama na mazao yake kutoka nje ya nchi.

**Madhumuni**
Kushirikiana na wadau kuhimiza usindikaji, uuzaji na ulaji wa nyama bora na mazao yake ili kufikia viwango vya lishe bora na kuongeza mauzo nje ya nchi.

**Tamko la Sera**
(i) Kwa kushirikiana na wadau, Serikali itawezesha na kuhimiza usindikaji, uuzaji na ulaji wa nyama bora na salama.
(ii) Serikali itadhibiti uingizaji na uuzaji wa nyama na mazao yake kutoka nje.
(iii) Serikali itahimiza ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko ya nyama na mazao yake.
(iv) Kwa kushirikiana na wadau, Serikali itawezesha na kuhimiza utafiti juu ya teknolojia ya nyama ili kukidhi mahitaji.

(v) Kwa kushirikiana na wadau, Serikali itahamasisha ulaji wa nyama bora na mazao yake.

(vi) Serikali itawezesha na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wasindikaji na walaji nyama pamoja na bodi itakayosimamia sekta ndogo ya nyama.

## 3.2 Maziwa

Uzalishaji wa maziwa ni moja ya shughuli za biashara inayokua haraka katika tasnia ya mifugo. Wanyama wanaofugwa kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa hapa nchini ni pamoja na ng'ombe, mbuzi, nyatimaji na ngamia. Maziwa mengi yanayouzwa hutokana na wafugaji wadogo ambao huzalisha takribani asilimia 70 na wafugaji wakubwa huzalisha karibu asilimia 30.

### 3.2.1 Ng'ombe wa Maziwa

Idadi ya ng'ombe wa maziwa nchini imeongezeka kutoka 212,000 mwaka 1995 na kufikia ng'ombe 500,000 mwaka 2005. Koo za ng'ombe wa maziwa zinazopatikana nchini ni pamoja na *Friesian, Jersey, Ayrshire, Sahiwal, Mpwapwa* na machotara wake. Mitamba ya ng'ombe wa maziwa nchini wanapatikana kwa wingi katika Mashamba ya Kuzalisha Mifugo (LMUs), taasisi za umma na mashamba madogo na makubwa ya watu binafsi.

Uzalishaji wa maziwa unakadiriwa kuwa lita bilioni 1.38 (mwaka 2005) ambapo ng'ombe wa asili walichangia kwa takribani asilimia 70. Wastani wa utoaji wa maziwa kwa mwaka kwa uzao kwa ng'ombe wa asili ni lita 500 ikilinganishwa na lita 2,000 kwa ng'ombe wa kisasa. Wafugaji wadogo wa ng'ombe wa maziwa wanapatikana kwa wingi katika maeneo ya mijini na maeneo ya viunga vya miji na vijijini katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Kagera, Dar es Salaam na Mbeya. Wastani wa unywaji maziwa kwa mtu kwa mwaka nchini ni lita 39 (mwaka 2005) ikilinganishwa na kiasi cha lita 200 kwa mtu kwa mwaka kinachopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO).

**Hoja**

Maendeleo ya tasnia ya maziwa nchini yanakabiliwa na vikwazo mbalimbali vikiwemo vya lishe duni, uhaba wa huduma za kitaalam na uchache wa ng'ombe wa maziwa. Vikwazo vingine ni pamoja na upatikanaji mdogo wa mitaji na mikopo, miundombinu duni ya kukusanya na kusambaza maziwa, viwanda vichache vya kusindika, unywaji mdogo wa maziwa na magonjwa ya mifugo.

**Madhumuni**

Kutumia rasilimali zilizopo kwa ajili ya uzalishaji kibiashara na unaozingatia mahitaji ya soko ili kuongeza kipato cha wadau wa maziwa na kuboresha hali ya maisha yao.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itahimiza uorodheshaji, uchambuzi, tathmini na uchaguzi wa koo bora za ng'ombe wa maziwa ili kuongeza tija.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza uboreshaji ukosaafu kwenye ng'ombe wa maziwa ili kuongeza tija.

(iii) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa.

(iv) Serikali itahamasisha matumizi ya teknolojia sahihi ya uzalishaji wa maziwa wenye tija.

(v) Juhudi zitafanyika kuhimiza uwekezaji katika uzalishaji, usindikaji na masoko ya maziwa.

(vi) Serikali itahamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya wazalishaji maziwa na kuimarisha Bodi ya Maziwa.

### 3.2.2 Mbuzi wa Maziwa

Kuanzishwa kwa ufugaji wa mbuzi wa maziwa nchini kumewezesha kuwepo kwa njia mbadala ya kupatikana kwa maziwa kwa kaya ambazo hazina uwezo wa kufuga ng'ombe wa maziwa. Pia, maziwa ya mbuzi ni lishe bora kwa wafugaji wenye uwezo mdogo.

Idadi ya mbuzi wa maziwa nchini inaongezeka hasa kupitia mpango wa "*kopa mbuzi lipa mbuzi".* Ufugaji wa mbuzi wa maziwa hufanywa na wafugaji wadogo, hususan wanawake na watoto. Aina ya mbuzi wa maziwa wanaofugwa ni pamoja na koo za *Toggenburg, Saanen, Anglo-Nubian, Alpine and Norwegian.*

**Hoja**

Ufugaji wa mbuzi wa maziwa unakabiliwa na vikwazo mbalimbali vikiwemo mbinu duni za ufugaji, magonjwa, uhaba wa koo bora za mbuzi, utafiti na huduma duni za ugani.

**Madhumuni**

Kuongeza uzalishaji wa mbuzi wa maziwa ili kukidhi mahitaji ya lishe na kuongeza kipato cha kaya.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itahimiza uorodheshaji, uchambuzi, tathmini na uchaguzi wa koo bora za mbuzi wa maziwa ili kuongeza tija.

(ii) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kuongeza uzalishaji wa mbuzi wa maziwa.

(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza uboreshaji ukosaafu kwenye mbuzi wa maziwa ili kuongeza tija.

(iv) Kwa kushirikiana na wadau, Serikali itahimiza na kuhamasisha unywaji wa maziwa bora na salama ya mbuzi.

(v) Juhudi zitafanyika kuhimiza na kuhamasisha ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi, katika mpango wa *'kopa mbuzi lipa mbuzi'*, uanzishwaji wa mitandao na vyama vya wafugaji wa mbuzi.

### 3.2.3 Nyatimaji na Ngamia

Nyatimaji na ngamia ni miongoni mwa wanyama wanaozalisha maziwa ingawa ni wachache nchini. Kuna nyatimaji wapatao 188 na ngamia 93 hapa nchini. Wanyama hawa wangeweza kuongeza upatikanaji wa maziwa katika maeneo ambayo mazingira hayaruhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa.

**Hoja**
Ufugaji wa nyatimaji na ngamia unakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uelewa na ujuzi mdogo kwa wafugaji na kuzaliana kinasaba kutokana na uchache wao.

**Madhumuni**
Kuongeza uzalishaji wa maziwa yatokanayo na nyatimaji na ngamia ili kuongeza kipato na lishe kwa kaya.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itahimiza na kuwezesha uboreshaji wa kosaafu na kuongeza idadi ya nyatimaji na ngamia.
(ii) Serikali itawezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kuongeza uzalishaji wa nyatimaji na ngamia.
(iii) Kwa kushirikiana na wadau, Serikali itahamasisha na kuhimiza unywaji wa maziwa bora na salama ya nyatimaji na ngamia.

### 3.2.4 Usindikaji, Masoko na Unywaji wa Maziwa

Miji na vituo vya biashara vimebakia kuwa soko kuu na la kutegemewa kwa maziwa yanayozalishwa vijijini. Hapa nchini kuna viwanda vidogo na kati 22 vya kusindika maziwa. Viwanda hivyo vina uwezo wa kusindika jumla ya lita 500,000 kwa siku, lakini kwa sasa husindika lita 150,000 tu, ambapo kiasi cha maziwa hayo huchanganywa na maziwa ya unga kutoka nje ya nchi.

**Hoja**
Usindikaji, uuzaji na unywaji/ulaji wa maziwa unakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na gharama kubwa za usindikaji na vifungashio, miundombinu duni ya uhifadhi na masoko, upungufu wa maziwa hasa wakati wa kiangazi, kutokuwa na utamaduni wa kunywa maziwa na vyama dhaifu vya wadau wa maziwa.

**Madhumuni**
Kushirikiana na wadau kuhimiza usindikaji, ufungaji, uuzaji na utumiaji wa maziwa na mazao yake ili kukidhi mahitaji ya soko la ndani na kuongeza mauzo nje.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza ukusanyaji na usindikaji wa maziwa yanayozalishwa nchini.
(ii) Kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya masoko ya maziwa.
(iii) Serikali itawezesha na kuimarisha asasi zinazosimamia zao la maziwa.
(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko na huduma za kitaalam.
(v) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itahamasisha na kuhimiza unywaji na utumiaji wa maziwa na mazao yake yanayozalishwa nchini.

## 3.3 Ngozi

Ngozi ni zao la ziada linalotokana na mifugo ambalo hutumika kama malighafi muhimu katika viwanda vya ngozi na huingiza fedha nyingi za kigeni. Idadi kubwa ya ngozi hutokana na mifugo ya asili. Uzalishaji wa ngozi kwa mwaka ni takribani vipande milioni 2.6 vya ng'ombe na vipande milioni 2.5 vya kondoo na mbuzi, ambapo asilimia 75 ya vipande hivyo hukusanywa. Aidha, inakadiriwa kuwa asilimia 95 ya ngozi zote huuzwa nje zikiwa ghafi hususan baada ya kukaushwa au kuwekewa chumvi.

**Hoja**
Ngozi kama zao muhimu la biashara halijatambuliwa na wafugaji wengi na hivyo kusababisha maendeleo duni ya tasnia ya ngozi. Ubora wa ngozi unakabiliwa na mbinu duni za ufugaji kama vile upigaji chapa ovyo, udhibiti hafifu wa wadudu wanaoshambulia wanyama na kuharibu ngozi pamoja na uchunaji, uhifadhi na usindikaji usioridhisha.

**Madhumuni**
Kuboresha uzalishaji, ukusanyaji na usindikaji wa ngozi kwa ajili ya soko la ndani na nje ili kuongeza kipato kutokana na zao la ngozi.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza upigaji mzuri wa chapa, uchinjaji, uchunaji uhifadhi na utunzaji mzuri wa ngozi.
(ii) Serikali itahimiza uuzaji wa ngozi kwa kuzingatia madaraja.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko ya ngozi na huduma za kitaalam.
(iv) Serikali itahimiza na kuimarisha udhibiti wa ubora wa zao la ngozi.
(v) Jitihada zitafanyika kuhimiza uwekezaji katika viwanda vya kusindika ngozi.

### 3.4 Mazao Mengine ya Ziada Yatokanayo na Mifugo

Mazao mengine ya ziada yatokanayo na mifugo na yenye umuhimu kiuchumi ni pamoja na sufu, damu, mifupa, pembe, kwato, manyoya na nywele za mifugo mbalimbali. Mazao hayo hutumika kwa madhumuni mbalimbali yakiwemo utengenezaji wa vyakula vya mifugo, madawa na mavazi.

**Hoja**

Uzalishaji na matumizi endelevu ya mazao ya ziada yatokanayo na mifugo yanakabiliwa na uelewa mdogo, kutokuwepo kwa miongozo na taratibu kuhusu uzalishaji, ukusanyaji, usindikaji na teknolojia sahihi.

**Madhumuni**

Kuhimiza uzalishaji na matumizi ya mazao ya ziada yatokanayo na mifugo kwa ajili ya malighafi ya viwanda na kuongeza kipato kwa wafugaji na wafanyabiashara.

**Tamko la Sera**

(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza uzalishaji na utumiaji wa mazao ya ziada yatokanayo na mifugo.
(ii) Serikali itahamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya ziada yatokanayo na mifugo.
(iii) Serikali itahimiza na kuwezesha utafiti kuhusu matumizi bora ya mazao ya ziada yatokanayo na mifugo.
(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha upatikanaji wa taarifa za masoko ya mazao ya ziada yatokanayo na mifugo na kutoa huduma za kitaalam.
(v) Serikali itahimiza na kuimarisha udhibiti wa ubora wa mazao ya ziada yatokanayo na mifugo.

### 3.5 Usimamizi wa Rasilimali za Nyanda za Malisho Katika Maeneo ya ufugaji na ukulima-ufugaji

Rasilimali ya Nyanda za Malisho inakadiriwa kuwa hekta milioni 60 na kati ya hizo, hekta milioni 40 zinatumika kwa malisho na hekta milioni 20 ni za vichaka na ardhi iliyopumzishwa. Rasilimali hiyo ina takribani uniti za mifugo (Livestock Units) milioni 17. Usimamizi bora wa nyanda za malisho na uzuiaji wa mbung'o utaweza kuongeza eneo la malisho litakaloweza kutosheleza takribani uniti za mifugo milioni 20. Usimamizi wa rasilimali za nyanda za malisho ni pamoja na matumizi, uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo.

#### 3.5.1 Matumizi ya Nyanda za Malisho

Utumiaji wa rasilimali za nyanda za malisho zilizopangwa na maeneo yaliyo wazi ni jambo la kawaida katika sehemu ambayo ardhi ipo kwa wingi. Wakati mwingine

maeneo haya humilikiwa na kusimamiwa na jumuiya au watu binafsi. Uchungaji wa mifugo katika ardhi inayomilikiwa kijumuiya huchangia kuwepo ufugaji wa kuhamahama kwa ajili ya kutafuta malisho na maji. Uhamaji huo husababisha kuenea kwa magonjwa ya mifugo, migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kuwepo kwa tabaka za kijamii, uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

**Hoja**

Matumizi ya nyanda za malisho kwa ajili ya ufugaji endelevu yanakabiliwa na mabadiliko ya kimsimu katika ubora na uwingi wa malisho, uchomaji moto ovyo, mifugo mingi kuzidi uwezo wa ardhi ya malisho, kutotengwa kwa maeneo ya malisho na kuwepo kwa mbung'o na kupe. Vilevile, matumizi endelevu ya nyanda za malisho hukwamishwa na udhaifu wa vyama vya wachungaji-wahamaji na wakulima-wafugaji, huduma duni za mifugo, ukosefu wa mikopo, huduma duni za kiuchumi, kijamii na miundombinu.

**Madhumuni**

Kuboresha usimamizi na matumizi ya nyanda za malisho ili kuwa na tija endelevu katika mifugo na maisha ya wachungaji-wahamaji na wakulima-wafugaji.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itahamasisha uorodheshaji, utambuzi, ulinzi, usimamizi na matumizi ya rasilimali nyanda za malisho.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itawezesha na kuimarisha huduma za kitaalam juu ya usimamizi wa nyanda za malisho.
(iii) Jitihada zitafanywa kuanzisha na kuendeleza miundombinu ya mifugo katika maeneo ya nyanda za malisho.
(iv) Matumizi sahihi ya njia za kuhifadhi malisho kwa ajili ya ulishaji wakati wa kiangazi yatahamasishwa.
(v) Serikali itaimarisha mfumo wa utoaji taarifa za awali kuhusu tishio la majanga na uhaba wa malisho.
(vi) Jitihada zitafanyika kuhamasisha na kuwezesha uanzishwaji wa vyama vya wafugaji-wahamaji na wakulima-wafugaji.

### 3.5.2 Uzalishaji wa Malisho na Mbegu.

Malisho yaliyostawishwa ni chanzo kimojawapo cha chakula cha mifugo. Hivi sasa kuna mashamba mawili ya umma na manane ya watu binafsi yanayotumika kama vyanzo vya mbegu za malisho. Mbegu hizo zinaweza kutumika kuboresha rasilimali ya nyanda za malisho ya asili. Wingi na ubora wa malisho haya pia hubadilika kufuatana na msimu ambapo wakati wa kiangazi hupungua na kuongezeka wakati wa masika.

**Hoja**
Uzalishaji wa malisho na mbegu unaathiriwa na uhaba wa mbegu bora, mvua zisizoaminika, elimu duni ya wafugaji na bei kubwa ya zana za kilimo.

**Madhumuni**
Kuongeza na kuboresha uzalishaji wa malisho na mbegu kwa ajili ya uzalishaji endelevu na wenye tija.

**Tamko la Sera:**
(i) Serikali itahamasisha matumizi ya malisho na mbegu bora za malisho.
(ii) Jitihada zitafanyika kuanzisha, kuhamasisha na kuimarisha mashamba ya mbegu bora za malisho pamoja na uzalishaji wa malisho na mbegu kwa njia ya umwagiliaji.
(iii) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam katika uzalishaji wa malisho na mbegu.
(iv) Jitihada zitafanyika kuhamasisha na kuwezesha vyama vya wadau katika uzalishaji malisho na mbegu za malisho.

### 3.5.3 Masalia ya Mazao

Tanzania inazo kanda mbalimbali za ikolojia za kilimo ambazo zinafaa kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka na jamii ya kunde. Mazao hayo ni vyanzo muhimu vya masalia ya kulisha mifugo hususan wakati wa kiangazi. Masalia hayo ni pamoja na mabua ya mahindi na mtama; maganda ya mazao ya nafaka na maharage; na vichungi na makapi ya miwa.

**Hoja**
Matumizi ya masalia ya mazao yanaathiriwa na elimu duni ya matumizi yake, uhaba wa teknolojia ya kuyahifadhi, viini lishe duni, upotevu wa masalia hayo baada ya mavuno, gharama kubwa ya kusafirisha inayotokana na ujazo mkubwa wa masalia.

**Madhumuni**
Kuhimiza hifadhi na matumizi sahihi ya masalia ya mazao ili kuongeza uzalishaji na tija katika mifugo.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhamasisha na kuhimiza matumizi ya masalia ya mazao yenye ubora.
(ii) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam katika matumizi ya masalia ya mazao.

### 3.5.4 Hifadhi ya Malisho

Mavuno ya malisho katika sehemu za tropiki hutofautiana kwa wingi na ubora kutegemeana na aina, ukomavu, hali ya hewa, rutuba ya udongo na matunzo. Majani na mitimalisho yaliyovunwa huhifadhiwa ili kutumika wakati wa upungufu wa malisho.

**Hoja**
Uzalishaji wa hei ni njia ya kawaida na rahisi katika kuhifadhi malisho hapa nchini. Aidha, utengenezaji wa sileji ni njia nyingine ya kuhifadhi malisho, lakini haitumiki sana kutokana na upungufu wa zana za kilimo, stadi za kazi na miundombinu duni . Hifadhi ya malisho inaathiriwa na mabadiliko ya hali ya hewa, uzalishaji hafifu na uelewa mdogo wa mbinu za uhifadhi.

**Madhumuni**
Kuhimiza hifadhi ya malisho na kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha mifugo wakati wa upungufu wa malisho ili kuongeza tija katika uzalishaji wa mifugo.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itahimiza uorodheshaji wa vyakula vya mifugo kwa lengo la kuvihifadhi.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza matumizi ya teknolojia sahihi katika kuhifadhi malisho.
(iii) Serikali itahimiza na kuimarisha huduma za kitaalam katika hifadhi ya malisho.
(iv) Serikali itaimarisha mfumo wa tahadhari (Livestock Early Warning System - LEWS) ili kukabiliana na upungufu wa malisho ya mifugo.

### 3.5.5 Maji kwa Matumizi ya Mifugo

Upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo ya wafugaji-wahamaji na wakulima-wafugaji hutokana na vyanzo vya aina mbili ambavyo ni maji yaliyo chini na juu ya ardhi. Maji yaliyo chini ya ardhi ni pamoja na; visima vifupi na virefu ambapo maji yaliyo juu ya ardhi hutokana na chemchemi, mito, mabwawa na malambo.

Zaidi ya asilimia 70 ya mifugo inapatikana katika maeneo kame ya Kanda ya Kaskazini, Kati na Magharibi ya Tanzania. Maeneo hayo yana upungufu mkubwa wa maji wakati wa kiangazi na hivyo huwalazimu wafugaji kuhama pamoja na mifugo yao kutafuta maji. Uhamaji huo husababisha upungufu mkubwa wa majani/malisho, uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na kuwepo sehemu chache zenye maji.

**Hoja**
Upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo ya wafugaji unaathiriwa na upungufu wa utaalam wa kuvuna maji, gharama kubwa za uchimbaji wa

mabwawa na zana za ujenzi, usambazaji witiri wa vyanzo vya maji na udhaifu wa vyama vya watumiaji maji.

**Madhumuni**
Kuanzisha, kutumia na kutunza vyanzo vya maji vya uhakika kwa ajili ya mifugo.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine italinda maeneo ya vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahimiza na kuwezesha ujenzi na utunzaji wa vyanzo ya maji kwa ajili ya mifugo.
(iii) Jitihada zitafanyika kuwezesha na kuimarisha uundaji wa kamati na vyama vya watumiaji maji.
(iv) Jitihada zitafanyika kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi za kuvuna maji kwa ajili ya mifugo.

## 3.6 Vyakula vya Viwandani

### 3.6.1 Vyakula Vilivyoongezewa Virutubisho

Vyakula vya mifugo vilivyoongezewa virutubisho vya protini, wanga, madini na vitamini ni muhimu katika uzalishaji mifugo, hususan kuku, maziwa na nguruwe. Vyakula hivyo huchangia takribani asilimia 60 ya gharama zote za uzalishaji wa mifugo. Uzalishaji wa mifugo wenye tija hutegemea upatikanaji wa vyakula vyenye viinilishe muhimu katika lishe. Uzalishaji wa vyakula vilivyosindikwa unakadiriwa kuwa tani 500,000 kwa mwaka ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 2.5.

**Hoja**
Uzalishaji wa vyakula vilivyoongezewa virutubisho unaathiriwa na uhafifu wa viungio, upatikanaji wa malighafi kwa msimu, uhaba wa mikopo, uelewa mdogo kuhusu uchanganyaji wa vyakula, gharama kubwa za uzalishaji na udhaifu wa vyama vya wasindikaji.

**Madhumuni**
Kuhimiza uzalishaji wa vyakula vya kusindika kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mifugo wenye tija.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza kilimo cha mazao mbalimbali kwa ajili ya malighafi ya kutengeneza vyakula vya mifugo.
(ii) Serikali itahimiza uanzishwaji wa viwanda vya kusindika vyakula vya mifugo vilivyoongezewa virutubisho.
(iii) Serikali itadhibiti ubora wa vyakula vya mifugo vitakavyotengenezwa nchini na vitakavyoagizwa kutoka nje.

(iv) Jitihada zitafanyika kuhimiza na kuwezesha uanzishwaji wa vyama vya wasindikaji wa vyakula vya mifugo vilivyoongezewa virutubisho.

### 3.6.2 Viungio vya Vyakula vya Mifugo

Matumizi ya viungio katika vyakula vya mifugo yanaongezeka, hususan katika ufugaji shadidi wa ng'ombe wa maziwa, kuku na nguruwe. Viungio hivyo hutumika kuboresha uzalishaji wa maziwa, ukuaji, ufanisi wa matumizi ya chakula mwilini na kinga ya magonjwa. Viungio hivi ni pamoja na; vimeng'enya, viini vya kuhamasisha kasi ya ukuaji, viua na vilinda vimelea vya sumu. Viungio vingi vya vyakula vya mifugo huagizwa kutoka nje ya nchi.

**Hoja**

Matumizi ya vichanganyo ya vyakula vya mifugo yanaathiriwa na ujuzi mdogo wa wafugaji na gharama kubwa za vyakula hivyo.

**Madhumuni**

Kuhimiza matumizi razini ya vichanganyo kwenye vyakula vya mifugo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mifugo wenye tija.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itaimarisha utoaji huduma za kitaalam kuhusu vichanganyo vya vyakula vya mifugo.
(ii) Jitihada zitafanyika kuhimiza uwekezaji katika kuzalisha vichanganyo vya vyakula vya mifugo nchini.

## 3.7 Uwiano wa Mifugo na Malisho

Mojawapo ya kanuni muhimu za ufugaji endelevu ni kuzingatia uwiano wa mifugo na malisho. Hata hivyo, mila na desturi kwa baadhi ya wafugaji ni kuwa na idadi kubwa ya mifugo kama ufahari na uhakika wa kuendelea kuwa na akiba ya mifugo. Hali hii husababisha kuwa na mifugo mingi kuliko uwezo wa ardhi na malisho.

Sababu ya pili ya kufuga bila kuzingatia uwiano huu ni uhamaji unaofanywa na wafugaji kutoka sehemu moja hadi nyingine kutokana na ukame wa mara kwa mara. Aidha, upanuzi wa kilimo na shughuli za wanyamapori, kuwepo kwa mbung'o, pia huchangia kupungua kwa maeneo ya malisho.

**Hoja**

Uwiano wa mifugo na malisho unaathiriwa na utumiaji mdogo wa mbinu bora za ufugaji, malisho ya asili duni, ukosefu wa ujasiriamali, ukosefu wa mfumo wa utoaji tahadhari ya majanga, sehemu chache za kunywea maji, tija ndogo ya mifugo ya asili, ukosefu wa vitega uchumi mbadala sehemu za vijijini na uhaba wa miundombinu ya masoko.

**Madhumini**
Kuhimiza ufugaji unaozingatia uwiano wa mifugo na malisho kwa ajili ya uzalishaji endelevu.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itahimiza ufugaji kulingana na uwezo wa ardhi na malisho.
(ii) Jitihada zitafanyika kuhimiza uboreshaji wa nyanda za malisho.
(iii) Serikali itaimarisha utoaji huduma za kitaalam kuhusu uwiano wa mifugo na malisho.
(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itahimiza uendelezaji wa vyanzo vya maji kwa mifugo.
(v) Serikali itahimiza uboreshaji wa kosaafu za mifugo ya asili
(vi) Serikali itaimarisha ufuatiliaji na udhibiti katika kuhamisha mifugo.

## 3.8 Wanyama-kazi

Idadi kubwa ya ng'ombe waliopo wanaweza kutumika kama nguvu kazi na kuchangia kuendeleza kilimo cha mazao, usafirishaji na nishati. Wanyama-kazi wengine ni pamoja na punda, ngamia, farasi, na nyatimaji.

### 3.8.1 Nguvu-kazi ya Wanyama

Matumizi ya wanyama-kazi ni teknolojia sahihi, rahisi na endelevu inayoweza kuchangia katika uzalishaji wa mazao ya kilimo. Matumizi ya wanyama-kazi hupunguza kwa takribani asilimia 75 ya harubu ya kazi katika kulima, kupanda na kupalilia. Inakadiriwa kuna wanyama-kazi milioni moja hapa nchini.

**Hoja**
Matumizi ya wanyama-kazi yanaathiriwa na upungufu wa maarifa na ujuzi mdogo wa wakulima, mbinu duni za ufugaji, uhaba na bei kubwa ya zana sahihi za kilimo.

**Madhumuni**
Kuhimiza uzalishaji na matumizi ya wanyama-kazi katika jamii kwa ajili ya nguvu-kazi.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza uzalishaji na matumizi ya wanyama-kazi.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itahimiza na kuwezesha uzalishaji na uchaguaji wa wanyama-kazi wenye sifa.
(iii) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam kwa ajili ya kuendeleza ya wanyamakazi.

### 3.8.2 Zana za Mifugo

Uzalishaji mifugo unahitaji mitambo, zana na vifaa maalum kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile ujenzi wa malambo, mashine za kukamulia, kulishia, utibabu, kusindika vyakula na mazao mbalimbali yatokanayo na mifugo pamoja na kutupa taka.

**Hoja**
Matumizi ya mitambo na zana za mifugo huathiriwa na uhaba na gharama kubwa za ununuzi, uzalishaji wa kujikimu wa mifugo, upungufu wa ujuzi na maarifa kwa wafugaji katika matumizi na matengenezo ya zana hizo.

**Madhumuni**
Kuhimiza matumizi ya zana za mifugo ili kuongeza ufanisi na tija katika mifumo ya uzalishaji mifugo.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza matumizi ya mitambo, zana na vifaa vya mifugo.
(ii) Serikali itahimiza uwekezaji katika kutengeneza mitambo, zana na vifaa vya mifugo.
(iii) Serikali itaimarisha huduma za kitaalamu kwenye matumizi ya mitambo, zana na vifaa vya mifugo.

### 3.8.3 Samadi na Biogesi

Wanyama hutoa kinyesi na mkojo kama mabaki ya lishe baada ya mmeng'enyo wa chakula mwilini. Mabaki mengine yanatokana na shughuli za machinjioni. Samadi inatokana na kuvunda kwa kinyesi ambacho huzalisha nishati ya biogesi ambayo inaweza kuhuishwa. Vilevile, samadi hutumika kama mbolea katika uzalishaji wa mazao na malisho. Matumizi ya biogesi huhifadhi mazingira kwani hupunguza matumizi ya kuni na hivyo hupunguza ukataji wa miti na pia inakuza kilimo hai.

**Hoja**
Matumizi ya samadi yanaathiriwa na ujazo mkubwa wakati wa kusafirisha, uelewa mdogo katika matumizi na hifadhi yake pamoja na mifumo ya ufugaji huria. Aidha, matumizi ya biogesi yanakwamishwa na uelewa mdogo kuhusu matumizi yake, gharama kubwa za uwekezaji katika teknolojia hiyo na upungufu wa wataalamu wenye fani katika ujenzi na ufungaji wa mitambo ya biogesi.

**Madhumuni**
Kuhimiza uzalishaji na matumizi ya samadi na biogesi ili kuboresha maisha ya wafugaji na kuhifadhi mazingira.

**Tamko la Sera**

(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza matumizi ya samadi katika mashamba ya mazao na malisho.

(ii) Jitihada zitafanyika kuhimiza ukusanyaji na utunzaji wa samadi na rojorojo yake.

(iii) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam katika uzalishaji na utumiaji wa samadi na biogesi.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza uwekezaji katika vifaa vya kuzalishia biogesi.

## 3.9 Uendelezaji wa Uzazi wa Mifugo

Koo bora za mifugo ni nyenzo muhimu katika kuongeza tija ya uzalishaji mifugo. Mifugo mingi iliyopo nchini ina ukosaafu mdogo unaosababisha kuwa na tija ndogo katika uzalishaji. Hata hivyo, baadhi ya wanyama hao wanazo sifa bainifu kama vile uwezo wa majike kulea vizuri, kuzaa sana na kukua haraka. Uboreshaji wa kosaafu za wanyama hawa unaweza kuongeza tija. Kupatikana kwa ukoo wa ng'ombe aina ya Mpwapwa na mbuzi aina ya "Blended" ni mifano mizuri wa jitihada hizi.

**Hoja**

Uendelezaji wa uzazi wa mifugo unaathiriwa na upungufu wa wataalamu, miundombinu duni, uhaba wa kosaafu zilizoendelezwa, ukosefu wa vyama na vikundi vya kuzalisha vizazi vya mifugo.

**Madhumuni**

Kuimarisha uendelezaji wa kosaafu za mifugo ili kuongeza uzalishaji wa mifugo yenye tija.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itahimiza uorodheshaji na uchambuzi wa koo za mifugo, tathmini na uboreshaji kosaafu.

(ii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kuendeleza uzazi wa mifugo.

(iii) Jitihada zitafanyika kuhimiza uanzishwaji wa vyama na vikundi vya kuzalisha vizazi vya mifugo ili kuwa na uhifadhi endelevu wa vizazi hivyo.

## 3.10 Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo

Utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo ni nyenzo muhimu katika uzalishaji wenye tija na faida kwa mifugo na mazao yake katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Utaratibu huu huhusisha utambuzi, usajili na ukusanyaji wa takwimu mbalimbali za mnyama kwa kipindi chote cha uhai wake ili kuwezesha ufuatiliaji. Takwimu hizi ni pamoja na tarehe, mahali alipozaliwa, ukoo wake, jinsia, uhamaji, afya na kumbukumbu nyingine za uzalishaji ili kuwezesha ufuatiliaji wa mnyama

na mazao yake. Kwa hivi sasa hakuna mfumo wa kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo.

**Hoja**
Utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake nchini vinakabiliwa na kukosekana kwa mfumo wa kitaifa, uduni wa miundombinu na vifaa, upungufu wa taaluma na uelewa mdogo miongoni mwa wadau wa Sekta ya Mifugo.

**Madhumuni**
Kuwa na mfumo wa kitaifa wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo ili kuongeza tija katika uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaanzisha mfumo wa kitaifa wa kutambua, kusajili na kufuatilia mifugo na mazao yake.

(ii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam kwa ajili ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake.

(iii) Jitihada zitafanyika kuhimiza na kuhamasisha kuhusu utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake.

## 3.11 Huduma za Utabibu wa Mifugo

Utoaji wa huduma bora za utabibu wa mifugo sharti uzingatie viwango, maazimio na miongozo mbalimbali vya Shirika la Afya ya Wanyama Ulimwenguni (OIE) kuhusu afya na udhibiti wa magonjwa ya wanyama na biashara yake kimataifa. Biashara ya mifugo na mazao yake inaongozwa na makubaliano ya kimataifa ya ukaguzi wa afya ya wanyama na mimea (Sanitary and Phytosanitary - SPS) chini ya Shirika la Biashara la Kimataifa (WTO).

Huduma za utabibu wa wanyama hujumuisha afya, ya mifugo, udhibiti na utokomezaji wa magonjwa ya mlipuko; wadudu na magonjwa yaenezwayo na wadudu; magonjwa mengine ya mifugo yenye athari za kiuchumi; ukaguzi wa mifugo na mazao yake; afya ya jamii kuhusiana na mifugo na usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo.

### 3.11.1 Utoaji wa Huduma za Afya ya Mifugo

Lengo kubwa la huduma za afya ya mifugo ni kudhibiti, kuzuia na kutokomeza magonjwa ya mifugo. Serikali ina jukumu la kudhibiti magonjwa ya mlipuko ya mifugo na yale yenye athari kwa binadamu na kiuchumi. Halikadhalika, sekta binafsi na wadau wengine wana jukumu la kudhibiti magonjwa yasiyo ya mlipuko na yenye athari ndogo kiuchumi. Sekta binafsi inahusika na kuagiza na kusambaza dawa za mifugo na pembejeo nyingine muhimu zinazohitajika na sekta.

**Hoja**
Utoaji wa huduma za afya ya mifugo unaathiriwa na udhaifu wa sekta binafsi, miundombinu duni, gharama kubwa za dawa na pembejeo, uhaba wa huduma za kitaalam na kiwango cha chini cha matumizi ya teknolojia.

**Madhumuni**
Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya mifugo ili kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo na hivyo kupunguza hasara na kuongeza tija.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza sekta binafsi kutoa huduma za utabibu wa mifugo na kuimarisha ushirikiano wa sekta za umma na binafsi katika kutoa huduma hizo.
(ii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam za afya ya mifugo.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahamasisha na kuhimiza uwekezaji katika uzalishaji wa madawa na pembejeo za mifugo.

## 3.11.2 Magonjwa ya Mlipuko kwa Mifugo

Magonjwa ya mlipuko kwa mifugo ni yale yanayoenea kwa kasi na yanayotakiwa kutolewa taarifa na kuchukuliwa hatua za kuyadhibiti mapema iwezekanavyo kabla hayajaleta madhara makubwa ndani na nje ya nchi. Ushirikiano wa kitaifa na kimataifa unahitajika katika kudhibiti magonjwa haya kwa kuwa na mfumo thabiti wa tahadhari, kutambua, kuratibu na kuoanisha mikakati ya udhibiti.

Magonjwa ya mlipuko yanayotokea mara kwa mara hapa nchini ni pamoja na Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Kichaa cha Mbwa, Ugonjwa wa kwato na Midomo na Homa ya Mapafu ya Mbuzi. Magonjwa mengine ni pamoja na Mdondo wa Kuku, Mapele Ngozi na Homa ya Nguruwe. Magonjwa ya mlipuko ambayo bado ni tishio ni kama Sotoka, *Pestes des Petits Ruminants* (PPR) na Mafua Makali ya Ndege**.**

**Hoja**
Udhibiti wa magonjwa ya mlipuko kwa mifugo unakwazwa na huduma hafifu za afya ya mifugo, miundombinu duni, udhaifu wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya ya mifugo, bei kubwa ya chanjo na uelewa mdogo wa wadau kuhusu magonjwa hayo.

**Madhumuni**
Kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mlipuko ili kuendeleza tasnia ya mifugo na upatikanaji wa masoko.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam katika kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mlipuko kwa mifugo.

(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahamasisha na kuhimiza uwekezaji katika kuzalisha chanjo na pembejeo za mifugo.
(iii) Serikali itaimarisha miundombinu kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko kwa mifugo.
(iv) Jitihada zitafanyika za kuoanisha sera za kitaifa na kimataifa za kuzuia na kutokomeza magonjwa ya mlipuko kwa mifugo.

### 3.11.3 Wadudu-ambukizi na Magonjwa Waenezayo

#### (a) Kupe na Magonjwa Wanayoeneza

Kupe na magonjwa wanayoeneza ni miongoni mwa vikwazo vikubwa vinavyoathiri ufugaji nchini. Inakadiriwa kuwa asilimia 72 ya vifo vyote vya ng'ombe nchini hutokana na magonjwa yanayoenezwa na kupe yakiwemo Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Maji Moyo na Mkojo Mwekundu.

**Hoja**
Vikwazo vikubwa katika udhibiti wa kupe na magonjwa wanayoeneza ni pamoja na gharama kubwa ya matibabu na dawa za kuogesha, upungufu wa huduma za kitaalam, usugu wa kupe kwa madawa ya kuogesha na uchungaji wa kuhamahama.

**Madhumuni**
Kudhibiti kupe na kutokomeza magonjwa wanayoeneza ili kuongeza uzalishaji wa mifugo na tija.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kudhibiti kupe na magonjwa wanayoeneza.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha miundombinu ya kudhibiti kupe na magonjwa wanayoeneza.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahamasisha na kuhimiza uwekezaji katika kuzalisha dawa za kuogesha, tiba pamoja na pembejeo nyinginezo za mifugo.

#### (b) Mbung'o na Nagana

Mbung'o wameenea katika maeneo mengi nchini na hivyo kuwa kikwazo katika matumizi ya ardhi ya malisho kwa ajili ya kuendeleza uzalishaji wa mifugo. Inakadiriwa kuwa kati ya hekta milioni 60 za ardhi inayofaa kwa ufugaji asilimia 40 imeenea mbung'o. Mbung'o hueneza ugonjwa wa nagana ambao huathiri afya ya mifugo na kuwa kikwazo cha kupanuka kwa uzalishaji mifugo.

**Hoja**

Udhibiti wa mbung’o na nagana unaathiriwa na uhamaji wa mifugo usiodhibitiwa, kuwepo kwa wanyamapori katika nyanda za malisho, gharama kubwa ya teknolojia ya kudhibiti mbung’o, usugu wa viuatilifu na uhaba wa wataalamu.

**Madhumuni**
Kudhibiti na kutokomeza mbung’o na nagana ili kuongeza uzalishaji wa mifugo wenye tija.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam katika kudhibiti mbung’o na nagana.
(ii) Kwa kushirikiana na wadau serikali itaimarisha miundombinu ya kudhibiti mbung’o na nagana.
(iii) Serikali itashirikiana na wadau kuhamasisha na kuhimiza uwekezaji katika uzalishaji wa viuatilifu na pembejeo nyingine za mifugo.
(iv) Jitihada zitafanyika za kuoanisha sera za kitaifa na kimataifa zinazohusu kuzuia na kutokomeza mbung’o.

### 3.11.4 Magonjwa Mengine ya Mifugo

Yapo magonjwa mengine yenye athari kiuchumi katika uzalishaji wa mifugo ambayo ni pamoja na magonjwa ya Kiwele, Chambavu, Haemorrhagic Septicemia, Nairobi sheep disease, Blue-tongue, Malignant Catarrhal Fever, minyoo pamoja na magonjwa ya ngozi, uzazi, na yale yanayosababishwa na ukosefu wa virutubisho.

Aidha, yapo magonjwa yanayoibuka ambayo yana athari kubwa kiuchumi na kwa afya ya binadamu. Magonjwa haya yanayoambukiza zaidi wanyama wakubwa ni pamoja na Homa ya Bonde la Ufa, Kichaa cha Ng’ombe, Caprine Arthritis Encephalitis, Hog Cholera, na Mafua ya Nguruwe.

Kwa upande wa kuku magonjwa mengine muhimu ni pamoja na Marek’s, Homa ya matumbo, Mycoplasma, Ndui ya Kuku, Gumboro, Koksidia, mafua ya kuku, kipindupindu cha kuku, minyoo, utitiri, chawa na ukurutu wa kuku. Kundi hili la magonjwa husababisha kwa kiwango kikubwa upungufu wa uzalishaji na tija katika mifugo.

**Hoja**
Udhibiti wa magonjwa yenye umuhimu kiuchumi unaathiriwa na uhaba wa watoa huduma za afya ya mifugo, miundombinu duni, udhaifu wa sekta binafsi, bei kubwa za dawa, chanjo na pembejeo, uelewa mdogo wa wadau kuhusu athari za magonjwa hayo kiuchumi.

**Madhumuni**
Kudhibiti na kutokomeza magonjwa ya mifugo yenye umuhimu kiuchumi ili kuongeza uzalishaji wa mifugo na tija.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kudhibiti magonjwa ya mifugo yenye umuhimu kiuchumi.
(ii) Kwa kushirikiana na wadau serikali itaimarisha miundombinu ya kudhibiti magonjwa ya mifugo yenye umuhimu kiuchumi.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahimiza na kuhamasisha wawekezaji katika kutengeneza dawa, chanjo na pembejeo nyinginezo za mifugo.
(iv) Jitihada zitafanyika za kuoanisha sera za kitaifa na kimataifa zinazohusu magonjwa ya mifugo yenye umuhimu kiuchumi.

### 3.11.5 Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake

Huduma za ukaguzi wa mifugo na mazao yake ni muhimu katika kudhibiti uingizaji na usambazaji wa magonjwa kutokana na kusafirisha mifugo na mazao yake kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Ukaguzi na utoaji wa vibali vya afya ya mifugo na ubora wa mazao yake ni sharti la lazima katika biashara ya kimataifa. Huduma hizi hutolewa katika vituo vya kuingia na kutoka nchini, machinjioni, vituo vya ukaguzi, maeneo ya kupumzikia mifugo, vituo vya kutotolea vifaranga na minada ya mifugo.

**Hoja**
Huduma za ukaguzi wa mifugo na mazao yake zinaathiriwa na miundombinu duni, uhaba wa wataalamu na uelewa mdogo wa wadau.

**Madhumuni**
Kuboresha huduma za ukaguzi wa mifugo na mazao yake ili kuzuia kuingia na kuenea kwa magonjwa ya mifugo.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itaimarisha miundombinu ya utoaji huduma za ukaguzi wa mifugo na mazao yake.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaimarisha udhibiti wa usafirishaji wa mifugo na mazao yake.
(iii) Jitihada zitafanyika kuoanisha sera za kitaifa na kimataifa kuhusu ukaguzi wa mifugo na mazao yake.

### 3.11.6 Mfumo wa Maabara za Mifugo

Mfumo wa maabara za mifugo unajumuisha Maabara Kuu ya Mifugo-Temeke (CVL) na maabara za vituo vya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo vya Kanda (VICs) vya Temeke, Mpwapwa, Iringa, Arusha, Mwanza, Mtwara na Tabora. Vituo hivi hufanya uchunguzi wa mienendo ya magonjwa, utambuzi wa magonjwa, kuhakiki ubora wa dawa na chanjo pamoja na kuratibu kampeni za chanjo. Aidha, maabara za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Taasisi ya Utafiti wa

Wanyamapori (TAWIRI) na maabara binafsi ni sehemu ya mtandao wa mfumo wa maabara za mifugo nchini.

**Hoja**
Mfumo wa maabara za mifugo unaathiriwa na uhaba wa miundombinu, vifaa na wataalamu, uelewa mdogo wa wadau na muundo dhaifu wa kitaasisi.

**Madhumuni**
Kuwa na mfumo imara wa maabara za mifugo ambao utatoa huduma bora za maabara kwa ajili ya kudhibiti magonjwa na ubora wa bidhaa za mifugo.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha miundombinu na vifaa katika mfumo wa maabara za mifugo nchini.
(ii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika mfumo wa maabara za mifugo.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahimiza utoaji wa huduma za maabara za mifugo.

### 3.11.7 Magonjwa ya Mifugo Yanayoambukiza Binadamu na Usalama wa Vyakula Vitokanavyo na Mifugo.

Magonjwa muhimu ya mifugo yanayoambukiza binadamu ni Kichaa cha Mbwa, Ugonjwa wa Kutupa Mimba, Kifua Kikuu, Kimeta, Malale, Tegu wa Nguruwe na Ng'ombe na *Salmonellosis*. Usimamizi na udhibiti wa magonjwa hayo ni muhimu katika kulinda afya ya binadamu. Jukumu kama hilo kwa upande wa usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo pia hufanyika kwa lengo hilo.

**Hoja**
Usimamizi na uthibiti wa magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu na usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo unaathiriwa na uhaba wa miundombinu na vifaa, udhaifu wa huduma muhimu za kitaalam na uelewa mdogo kwa baadhi ya wadau.

**Madhumuni**
Kutoa huduma ya usimamizi na udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo ili kuwahakikishia walaji vyakula bora na salama.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha miundombinu na vifaa vya kutoa huduma ya usimamizi na udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo.

(ii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam kuhusu usimamizi na udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo.
(iii) Kwa kushirikiana na wadau wengine serikali itahimiza utoaji wa huduma ya usimamizi na udhibiti wa magonjwa ya mifugo yanayoambukiza binadamu na ubora wa vyakula vitokanavyo na mifugo.

### 3.12 Utafiti wa Mifugo

Utafiti wa mifugo unahusika na upatikanaji na uendelezaji wa teknolojia zinazolenga kutatua matatizo yanayoathiri tasnia ya mifugo ili kuongeza tija. Kwa wakati huu, utafiti unalenga ng'ombe wa maziwa na nyama, mbuzi, kondoo, wanyama wasiocheua, malisho, lishe ya mifugo, kosaafu za mifugo na magonjwa ya mifugo.

Utafiti wa mifugo nchini unafanyika katika vituo vifuatavyo: Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo (NLRI) - Mpwapwa, Kituo cha Utafiti wa Mifugo (LRC) – Tanga, Kituo cha Utafiti wa Mifugo (LRC) – West Kilimanjaro, Maabara Kuu ya Mifugo (CVL) – Temeke, Taasisi ya Utafiti wa Mbung'o na Ndorobo (TTRI) – Tanga na Kituo cha Utafiti wa Malisho (PRC) – Kongwa. Vilevile, Utafiti wa Mifugo unafanyika katika vituo vya Uyole, Tumbi, Selian, Naliendele na Ukiriguru. Pia, washiriki wengine katika utafiti wa mifugo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika nchi za Tropiki (TPRI), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) na Taasisi ya Utafiti wa Misitu (TAFORI).

**Hoja**
Utafiti wa mifugo unaathiriwa na gharama kubwa za uwekezaji, uhaba wa vifaa na miundombinu, upungufu wa wataalamu, uratibu hafifu wa shughuli za utafiti na ushiriki mdogo wa sekta binafsi.

**Madhumuni**
Kutafiti na kuendeleza teknolojia sahihi za tasnia ya mifugo ili kuongeza uzalishaji na tija.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha, itahimiza, itaendeleza na kuwezesha uwekezaji katika utafiti wa mifugo.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaimarisha miundombinu na vifaa kwa ajili ya utafiti wa mifugo.
(iii) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam kwa ajili ya utafiti wa mifugo.
(iv) Jitihada zitafanyika ili kuimarisha ushirikiano kati ya utafiti, ugani na wafugaji.
(v) Jitihada zitafanyika ili kuimarisha uratibu na ushirikiano wa wadau katika utafiti wa mifugo.

### 3.13 Bioteknolojia na Matumizi Salama

Bioteknolojia ni muhimu kwa uzalishaji endelevu katika tasnia ya mifugo na inapotumika pamoja na teknolojia nyingine za uzalishaji wa mifugo, huweza kusaidia kukabiliana na mahitaji yanayotokana na ongezeko la idadi ya watu.

Bioteknolojia hapa nchini, kwa wakati huu, inatumika kuhifadhi mbegu za vizazi; mbinu za uzazi kama vile uhamilishaji; uchunguzi wa magonjwa na utengenezaji wa chanjo. Hata hivyo, kwa siku zijazo bioteknolojia inaweza kutumika katika matumizi mbalimbali yakiwemo uhawilishaji viini tete, kubadilisha na kupandikiza vinasaba, uzalishaji wa virutubisho na vichanganyio katika vyakula vya mifugo.

**Hoja**
Licha ya matumizi mazuri ya bioteknolojia, bado kuna athari zinazoweza kujitokeza katika afya za binadamu na wanyama pamoja na mazingira. Matumizi ya bioteknolojia yanaathiriwa na uelewa mdogo wa jamii, uhaba wa utaalam, miundombinu na vifaa.

**Madhumuni**
Kuhamasisha matumizi ya bioteknolojia na matumizi salama ili kuboresha uzalishaji wa mifugo na kuongeza tija.

**Tamko la sera**
(i) Kwa kushirikiana na wadau wengine, Serikali itahamasisha matumizi ya bioteknolojia na matumizi salama.
(ii) Jitihada zitafanyika kuimarisha na kuendeleza utafiti wa matumizi ya bioteknolojia na matumizi salama.
(iii) Kwa kushirikiana na wadau, Serikali itaimarisha miundombinu na vifaa kwa ajili ya matumizi ya bioteknolojia na matumizi salama katika tasnia ya mifugo.
(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahamasisha na kuhimiza uwekezaji katika bioteknolojia na matumizi salama.
(v) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam kwa ajili ya kuendeleza bioteknolojia na matumizi salama.

### 3.14 Kilimo Hai katika Ufugaji

Kilimo hai katika ufugaji ni dhana mpya inayojitokeza katika uzalishaji wa mifugo na mazao unaohimiza kutotumia au matumizi kidogo ya kemikali za viwandani kama vile mbolea, viuatilifu na madawa. Dhana hii imetokana na matumizi mabaya ya madawa ya viwandani ambayo yanasababisha madhara ya kiafya kwa binadamu. Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la mahitaji duniani ya mazao yanayozalishwa kwa kuzingatia kilimo hai katika ufugaji.

**Hoja**
Kilimo hai katika ufugaji kinaweza kuwa chanzo cha kuipatia riziki jamii ya wafugaji ikiwa kitahimizwa na kuwezeshwa na Serikali na sekta binafsi. Hata hivyo, kutokana na uchanga wa kilimo hai katika ufugaji kunahitajika uwekezaji, utaalam na uhamasishaji ili uelewa na kukubalika kwake kuwe kwepesi.

**Madhumuni**
Kuhimiza uzalishaji wa mazao ya mifugo yatokanayo na kilimo hai katika ufugaji ili mazao yakidhi mahitaji maalum ya soko.

**Tamko la Sera**
(i) Kwa kushirikiana na wadau, Serikali itahimiza na kuhamasisha kilimo hai katika ufugaji.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itahamasisha na kuhimiza uwekezaji katika ufugaji wa kilimo hai.
(iii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam kuendeleza kilimo hai katika ufugaji.

## 3.15 Huduma za Ugani

Huduma za ugani katika mifugo zinahusisha uhawilishiaji wa teknolojia kutoka kwa wataalam kwenda kwa wafugaji na kubadilishana taarifa na uzoefu kati ya wadau ili kuongeza uzalishaji na tija. Njia mbalimbali katika utoaji wa huduma za ugani zimekuwa zikitumika zikiwemo: kutembelea wafugaji na kuwapa mafunzo, shamba darasa na uhamasishaji wa matumizi ya mazao. Njia nyingine ni pamoja na ziara za mafunzo, siku ya wakulima na wafugaji, vyombo vya habari, mafunzo ya wafugaji vyuoni, maonyesho ya wakulima na wafugaji na mashamba ya mafunzo.

Utoaji wa huduma za ugani ulikuwa ni jukumu la Serikali Kuu hadi kufikia mwaka 1990. Jukumu hilo kwa sasa ni la Serikali za Mitaa na Sekta binafsi ambapo Serikali Kuu imebakia na wajibu wa kuandaa sera, kutoa miongozo na ushauri wa kitaalamu.

**Hoja**
Utoaji wa huduma za ugani unakwamishwa na ushirikiano dhaifu miongoni mwa wadau; uhaba wa wataalamu; ushirikiano na uratibu dhaifu baina ya utafiti, ugani, mafunzo na wafugaji, pamoja na uhaba wa miundombinu na vifaa.

**Madhumuni**
Kutoa huduma bora za ugani zinazokidhi mahitaji ya wafugaji na wadau wengine.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itaimarisha uratibu wa watoa huduma za ugani wa mifugo katika ngazi zote.

(ii) Jitihada zitafanywa katika kuratibu na kuimarisha ushirikiano katika nyanja za utafiti, mafunzo, ugani na shughuli za ufugaji.
(iii) Serikali itashirikiana na wadau wengine kuimarisha miundombinu na vifaa vya utoaji huduma za ugani.
(iv) Serikali itahimiza na kuimarisha huduma shirikishi za ugani.
(v) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika ugani.

### 3.16 Mafunzo ya Mifugo

Utoaji wa mafunzo ya mifugo unahusisha kuandaa, kutekeleza, kuratibu, kufuatilia na kupitia programu za mafunzo kwa lengo la kupata wataalamu mahiri ili kuendeleza tasnia ya mifugo.

Hivi sasa, wizara ina jumla ya vyuo 6 vya mafunzo ya mifugo vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 970 kwa mwaka. Vyuo hivyo ni Tengeru, Mpwapwa, Morogoro, Madaba, Buhuri na Temeke. Vyuo vitano kati ya hivyo hutoa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya astashahada na stashahada pamoja na kufundisha wafugaji stadi mbalimbali za mifugo. Aidha, Chuo cha LITI Buhuri ni mahususi kwa kutoa mafunzo mafupi kwa ajili ya ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa. Washiriki wengine katika utoaji wa mafunzo ya mifugo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATIs), Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) na Asasi Zisizo za Kiserikali (NGOs).

**Hoja**
Utoaji wa mafunzo ya mifugo unaathiriwa na uhaba wa miundombinu, vifaa na wataalamu, ushiriki mdogo wa wadau wengine pamoja na ushirikiano na uratibu dhaifu baina ya utafiti, mafunzo, ugani na wafugaji.

**Madhumuni**
Kutoa wataalamu makini wa mifugo na wafugaji wenye ujuzi kwa ajili ya tasnia ya mifugo.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaboresha na kutunza miundombinu na vifaa vya mafunzo ya mifugo.
(ii) Serikali itahimiza vyuo vya mafunzo kujiendesha na kufikia hadhi ya viwango vya mafunzo vya kimataifa.
(iii) Jitihada zitafanyika kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa mafunzo.
(iv) Serikali itaimarisha ushirikiano katika nyanja za utafiti, mafunzo, ugani na shughuli za ufugaji.

### 3.17 Taarifa na Takwimu za Mifugo

Upatikanaji wa taarifa na takwimu za mifugo unahusisha ukusanyaji, uchambuzi, uhifadhi na usambazaji wake kwa ajili ya kuwezesha kupanga, kudhibiti, kuratibu na kutoa maamuzi mbalimbali. Taarifa na takwimu ni nyenzo muhimu katika uendeshaji hivyo ni muhimu ziwe timilifu, sahihi, zisizotofautina na zinazopatikana kwa wakati zinapohitajika.

**Hoja**

Upatikanaji wa taarifa na takwimu za mifugo nchini kutoka chanzo kimoja kilichoidhinishwa haujawa imara. Hali hii imesababisha kutokuwepo kwa takwimu rasmi za sekta ya mifugo.

Aidha, upatikanaji wa taarifa na takwimu za mifugo unaathiriwa na uhaba wa miundombinu na vifaa, gharama kubwa za ukusanyaji wa takwimu, uhaba wa wataalamu wenye ujuzi, ukosefu wa mfumo maalum wa upatikanaji na hifadhi ya takwimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara.

**Madhumuni**

Kutoa taarifa na takwimu sahihi kwa wadau kuhusu tasnia ya mifugo ili kuwezesha kupanga na kutoa maamuzi sahihi.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itaimarisha miundombinu na vifaa kwa ajili ya upatikanaji wa taarifa na takwimu za mifugo.
(ii) Jitihada zitafanyika ili kuoanisha na kuratibu taarifa na takwimu za mifugo.
(iii) Serikali itaimarisha huduma za kitaalam kwa ajili ya taarifa na takwimu za mifugo.
(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaanzisha mfumo imara wa kusimamia upatikanaji wa taarifa na takwimu za mifugo.
(v) Serikali itahakikisha na kuwezesha kufanyika kwa sensa mbalimbali za mifugo kwa wakati.

### 3.18 Dawa za Tiba na Kinga ya Wanyama

Dawa za tiba na kinga ya wanyama hujumuisha kemikali na chanjo zinazotumika kwa ajili ya kutibu, kuzuia na kutambua magonjwa ya wanyama ili kuongeza tija.

Utoaji wa dawa za wanyama unafanywa kwa sehemu kubwa na sekta binafsi. Serikali imebakia na jukumu la udhibiti na ufuatiliaji kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwa kushirikiana na Wizara.

**Hoja**
Matatizo yanayokabili matumizi ya dawa za mifugo ni pamoja na upatikanaji wake, gharama kubwa, uwezo mdogo wa kudhibiti ubora wa dawa, uelewa mdogo wa wadau kuhusu matumizi ya dawa na mtandao duni wa usambazaji.

**Madhumuni**
Kuhakikisha upatikanaji, usambazaji mzuri, bei nafuu na matumizi salama ya dawa bora za wanyama.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itahimiza na kuwezesha utengenezaji, uagizaji na usambazaji wa dawa bora za tiba ya wanyama.
(ii) Serikali itaimarisha utoaji huduma za kitaalam katika dawa za tiba ya wanyama.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha na kuhimiza uanzishwaji wa vikundi vya wadau vya kusambaza dawa za mifugo.

## 3.19 Ustawi wa Wanyama

Ustawi wa wanyama unahusu jinsi binadamu anavyomhudumia na kumpa haki za msingi mnyama yeyote anayesafirishwa, anayefugwa kwa matumizi mbalimbali ama anapoamua kusitisha uhai wake. Matumizi ya mnyama ni pamoja na kuchinja kwa madhumuni mbalimbali, kufanyia utafiti katika maabara, kutumika kama nguvukazi, kuwa mnyama rafiki na katika burudani. Kwa wakati huu, kuna asasi mbalimbali zisizo za kiserikali (NGOs) zinazojihusisha na ustawi wa wanyama.

**Hoja**
Ustawi wa wanyama nchini unaathiriwa na uelewa mdogo wa wadau juu ya huduma na haki zao, mila na desturi, ukosefu wa uratibu na vyombo duni vya kutoa huduma kwa wanyama.

**Madhumuni**
Kuhakikisha kuwa ustawi wa wanyama unazingatiwa na wadau wa mifugo kulingana na viwango vinavyokubalika.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhamasisha wadau wa mifugo kuhusu ustawi wa wanyama.
(ii) Serikali itaimarisha utoaji huduma za kitaalam kwa ajili ya ustawi wa wanyama.
(iii) Serikali itaimarisha uratibu miongoni mwa wadau wanaojihusisha na ustawi wa wanyama.

### 3.20 Maadili katika Utoaji wa Huduma za Utabibu wa Mifugo

Taaluma ya utabibu wa mifugo sharti izingatie miongozo inayotolewa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) kuhusu utoaji huduma za utabibu wa mifugo. Zaidi ya hapo, utoaji huduma za utabibu wa mifugo huhitaji kuzingatia maadili kama yalivyoainishwa kwenye miiko ya kazi zao.

Kwa wakati huu, utoaji wa huduma za afya ya mifugo upo katika kipindi cha mpito ambapo sekta binafsi inafanya kazi hizo sanjari na sekta ya umma.

**Hoja**

Usimamizi wa taaluma ya utabibu wa mifugo unaathiriwa na uwezo mdogo wa kufuatilia na kushauri, upungufu wa wataalamu, uhaba wa miundombinu na vifaa, uelewa mdogo wa wadau na udhaifu katika kuratibu shughuli za wadau wanaotoa huduma za utabibu wa mifugo.

**Madhumuni**

Kudhibiti taaluma ya utabibu wa mifugo ili kupata huduma bora za matibabu ya wanyama.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam katika kusimamia taaluma ya utabibu wa mifugo.
(ii) Serikali itaimarisha usimamizi wa huduma za utabibu wa mifugo unaozingatia viwango na maadili.
(iii) Serikali itahimiza uendelezaji wa taaluma na mawasiliano yanayohusu utabibu wa mifugo.

### 3.21 Ujuzi Asilia katika Kuendeleza Ufugaji

Ujuzi Asilia katika Kuendeleza Ufugaji (ITK) ni mkusanyiko wa elimu na stadi mbalimbali walizonazo watu katika maeneo yao, ambazo huzitumia kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Katika uendelezaji wa mifugo, ujuzi asilia huhusisha uzalishaji na utabibu wa mifugo, usimamizi wa nyanda za malisho na masuala ya mazingira.

Wafugaji walio wengi vijijini hutegemea, kwa kiwango kikubwa, ujuzi na stadi za asili katika kudhibiti magonjwa ya wanyama na kuongeza tija. Hii ni kwa sababu ujuzi asilia ni rahisi kupatikana na kutumiwa, una gharama nafuu na hauharibu mazingira. Maabara Kuu ya Mifugo-Temeke, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo-Mpwapwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo hutumika kama vituo maalum vya kuthibitisha matumizi ya madawa asilia ya kutibu mifugo.

**Hoja**
Ujuzi asilia unaathiriwa na ukosefu wa kumbukumbu, kutotambulika na jamii, kutosambazwa kwa ujuzi huo, uelewa mdogo miongoni mwa wadau, uhaba wa wataalamu, ukosefu wa viwango vya matumizi, uhaba wa miundombinu na vifaa.

**Madhumuni**
Kuhimiza matumizi ya ujuzi asilia ili kuongeza uzalishaji wa mifugo na tija.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam za ujuzi asilia.
(ii) Jitihada zitafanyika kuongeza uelewa miongoni mwa wadau kuhusu ujuzi asilia.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau itaimarisha miundombinu na vifaa kazi kwa ajili ya kuendeleza ujuzi asilia.
(iv) Serikali itahimiza ushirikiano kati ya sekta za umma na binafsi na miongoni mwa jamii husika kuhusu ujuzi asilia.

## 3.22 Wanyama Rafiki

Wanyama rafiki ni wale wenye uhusiano maalum na binadamu na ambao huchangia ubora wa maisha kwa wanaowafuga na hivyo huthaminiwa na jamii. Wanyama rafiki wanaofugwa ni pamoja na mbwa, paka, ndege na wanyama wengine wafugwao. Mahitaji ya wanyama rafiki walio bora yameongezeka nchini.

**Hoja**
Utunzwaji wa wanyama rafiki unaathiriwa na upatikanaji wa wanyama walio bora, matunzo hafifu, unyanyapaa, utaaalamu duni na uelewa mdogo.

**Madhumuni**
Kuhimiza utunzaji sahihi wa wanyama rafiki katika jamii.

**Tamko la Sera**
(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza matunzo ya wanyama rafiki na matumizi sahihi ya vifaa vya kuwatunzia.
(ii) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam kwa wanyama rafiki.
(iii) Jitihada zitafanyika kuongeza uelewa kuhusu wanyama rafiki miongoni mwa jamii.

## 3.23 Masuala ya Kisekta na Mtambuka

Maendeleo ya mifugo huguswa na masuala mengine yaliyo nje ya majukumu ya wizara. Masuala hayo ni pamoja na umilikaji ardhi, mazingira, jinsia, VVU/UKIMWI, miundombinu, rasilimali fedha na mikopo. Ili kuharakisha maendeleo ya mifugo, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine, itaanzisha mpango wa kuratibu na kuainisha masuala hayo.

### 3.23.1 Umiliki wa Ardhi kwa Ufugaji

Umiliki wa ardhi ni haki inayowezesha utumiaji wake kulingana na masharti yaliyoelekezwa. Masharti haya huwezesha kupata ardhi, kuhodhi, kutumia, kutoa, kuhamisha au kuachia umiliki. Ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa ufugaji hapa nchini kwa kiwango kikubwa hutumika kijumuia bila uhakika wa umiliki. Hali hii imesababisha migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uharibifu wa ardhi na kuenea kwa magonjwa ya mifugo.

**Hoja**
Umiliki wa ardhi kwa ajili ya mifugo unaathiriwa na uelewa mdogo miongoni mwa wadau kuhusu umuhimu wa umiliki ardhi kisheria na taratibu za upatikanaji wake, upungufu wa watalaamu na kutoweka kipaumbele katika kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji.

**Madhumuni**
Kuhakikisha matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya uzalishaji mifugo endelevu na wenye tija.

**Tamko la Sera**
(i) Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahimiza utoaji huduma za kitaalam kwa ajili ya matumuzi ya ardhi ya ufugaji.
(ii) Serikali itaweka taratibu za matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya uzalishaji mifugo.
(iii) Serikali kwa kushirikiana na wadau, itahimiza na kuwezesha uanzishwaji wa vyama vya wachungaji-wahamaji na wakulima-wafugaji.

### 3.23.2 Ufugaji Kandokando ya Miji

Ufugaji kandokando ya miji hufanyika karibu kwenye miji yote mikubwa na midogo nchini. Aina ya mifugo inayofugwa kwenye mfumo huu ni pamoja na ng'ombe na mbuzi wa maziwa, kuku na nguruwe. Mfumo huu wa uzalishaji, kama ukihimizwa una fursa kubwa ya kutoa ajira, kipato, vyanzo mbadala vya mazao ya mifugo kwa wakazi wa mijini.

**Hoja**
Ufugaji kandokando mwa miji unaathiriwa na upungufu wa ardhi, upatikanaji wa mifugo bora na pembejeo, migogoro katika jamii, upungufu wa wataalamu, uchafuzi wa mazingira na masoko yasiyo ya uhakika.

**Madhumuni**
Kuhimiza ufugaji wa kandokando mwa miji ili kuongeza ajira, kuinua kipato cha kaya na uhakika wa chakula.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam na kuhimiza ufugaji wa kandokando mwa miji.

(ii) Serikali itahamasisha na kuwezesha ufugaji wa kandokando mwa miji usioathiri mazingira.

### 3.23.3 Hifadhi ya Mazingira

Mazingira hujumuisha hewa, ardhi, maji, mimea, maisha ya binadamu na wanyama; na vipengele mbalimbali vinavyohusu uchumi, utamaduni na maisha ya jamii. Ufugaji endelevu na shughuli nyingine zinazohusiana nao zinahitaji matumizi sahihi na utunzaji wa mazingira.

**Hoja**

Ongezeko la mifugo na shughuli za kibinadamu zinazohusiana na uzalishaji wa mifugo katika baadhi ya maeneo nchini umesababisha matumizi makubwa ya maliasili. Hali hii imesababisha uchungaji uliokithiri, mmomonyoko wa ardhi, kutoweka kwa misitu, uharibifu wa vyanzo vya maji na mazingira.

Hifadhi ya mazingira katika uzalishaji wa mifugo inaathiriwa na uelewa mdogo wa wadau, kutopewa kipaumbele katika utengaji wa maeneo ya mifugo, upungufu wa wataalamu na udhaifu katika uratibu baina ya sekta mbali mbali.

**Madhumuni**

Kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa kwa ajili ya ufugaji endelevu.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itaimarisha utoaji wa huduma za kitaalam juu ya masuala ya mazingira.

(ii) Jitihada zitafanyika kuhimiza upangaji sahihi wa matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya uzalishaji wa mifugo.

(iii) Jitihada zitafanyika kuimarisha uratibu baina ya sekta mbali mbali kuhusu masuala ya mazingira.

### 3.23.4 Masuala ya Jinsia katika Tasnia ya Mifugo

Uhusishaji wa jinsia katika tasnia ya mifugo ni mkakati muhimu wa kuwahusisha wanawake na wanaume katika kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini sera na progamu za mifugo. Lengo ni kuhakikisha kuwa jinsia zote zinafaidika na sera na programu hizo na hakuna anayenyimwa haki. Pamoja na dhana hii kuwa mpya, imeanza kukubalika katika makundi mengi ya jamii ya wafugaji.

**Hoja**

Uhusishaji wa jinsia katika tasnia ya mifugo unaathiriwa na uelewa mdogo wa wadau, uhaba wa wataalamu, mila na desturi.

**Madhumuni**
Kuhakikisha masuala ya jinsia yanahusishwa kikamilifu ili kuwa na usawa wa kijinsia katika tasnia ya mifugo.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali itahimiza utoaji wa huduma za kitaalam kuhusu jinsia katika tasnia ya mifugo.
(ii) Serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine itaimarisha uhusishaji wa jinsia katika uendelezaji wa mifugo.

### 3.23.5 VVU/UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu

VVU/UKIMWI ni janga la kitaifa na kimataifa ambalo limesababisha matatizo miongoni mwa jamii husasan vijana wa kike na kiume. Mbali na VVU/UKIMWI, malaria na kifua kikuu ni miongoni mwa magonjwa hatari. Aidha, kulingana na Sera ya Taifa ya VVU/UKIMWI ya mwaka 2001, Tanzania ni miongoni mwa nchi za Kusini ya Jangwa la Sahara zilizoathirika sana na janga hili.

**Hoja**
VVU/UKIMWI, malaria and kifua kikuu husababisha upungufu wa nguvu kazi pamoja na wafugaji, hivyo huathiri uzalishaji mifugo. Pia, VVU/UKIMWI hupunguza sana raslimali za fedha kutokana na gharama za utambuzi na matibabu ya magonjwa nyemelezi. Jitihada za pamoja zinaelekezwa katika kuongeza uelewa wa jamii ili kuzuia maambukizi mapya.

Jitihada za kupambana na maambukizi ya VVU/UKIMWI katika sekta ya mifugo zinaathiriwa na vipengele mbalimbali vinavyohusu uchumi, utamaduni na maisha ya jamii, uelewa mdogo miongoni mwa jamii, uhaba wa miundombinu na vifaa hususan katika jamii za wachungaji-wahamaji.

**Madhumuni**
Kuchangia kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI, kifua kikuu na malaria miongoni mwa jamii ili kuongeza tija katika sekta ya mifugo.

**Tamko la Sera**

(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza ufahamu kuhusu VVU/UKIMWI, kifua kikuu na malaria miongoni mwa wadau wa sekta ya mifugo.
(ii) Serikali itaimarisha uhusiano na wadau wengine katika kuzuia VVU/UKIMWI, kifua kikuu na malaria miongoni mwa wadau wa mifugo.

### 3.23.6 Miundombinu

Miundombinu na nyenzo muhimu kwa ajili ya kuendeleza ufugaji ni pamoja na usafiri (reli maji, anga na barabara), mawasiliano, umeme, vifaa vya uhifadhi, majosho, minada, miundombinu ya maji, vituo vya kupumzikia mifugo na

karantini, njia za mifugo na machinjio. Kwa wakati huu, miundombinu iliyopo inamilikiwa na kuendeshwa na wadau mbalimbali.

**Hoja**

Matatizo yanayoathiri miundombinu ya mifugo ni pamoja na gharama kubwa za uwekezaji, uhaba na uchakavu wa miundombinu, uratibu na ushiriki mdogo wa sekta binafsi.

**Madhumuni**

Kuwa na miundombinu muhimu kwa ajili ya kuendeleza tasnia ya mifugo.

**Tamko la Sera**

(i) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itahamasisha na kuwezesha uwekezaji katika kujenga na kukarabati miundombinu kwa ajili ya kuendeleza ufugaji.

(ii) Serikali itaimarisha uratibu wa wadau wanaohusika katika uendelezaji wa miundombinu ya mifugo

### 3.23.7 Fedha na Mikopo

Uwekezaji katika tasnia ya mifugo huhitaji mitaji mikubwa ambayo wengi wa wajasiriamali wa mifugo hawana. Hata hivyo, mikopo mingi iliyopo ni ya muda mfupi, yenye riba kubwa ambayo haivutii wawekezaji kutokana na mashaka ya uwekezaji katika tasnia ya mifugo. Taasisi za fedha zinazowezesha uwekezaji kwenye tasnia ya mifugo ni pamoja na Benki za Biashara, Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOs) na Vyama vya Akiba na Mikopo (SACAs). Asasi nyingine zisizo rasmi ni kama vile "mpango wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe" na vikundi vya kuweka na kukopa vijijini.

**Hoja**

Upatikanaji wa fedha na mikopo kwa ajili ya tasnia ya mifugo unaathiriwa na riba kubwa, gharama kubwa za uwekezaji, faida huchukua muda mrefu kupatikana, mashaka makubwa yanayohusiana na shughuli za ufugaji, ukosefu wa bima ya mifugo, uhaba wa dhamana na uelewa mdogo baina ya wadau.

**Madhumuni**

Kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuwekeza katika tasnia ya mifugo.

**Tamko la Sera**

(i) Jitihada zitafanyika kuhimiza kuwepo kwa taasisi maalum za fedha za kutoa mikopo kwa ajili ya tasnia ya mifugo.

(ii) Jitihada zitafanyika kuhimiza kuwepo kwa bima ya mifugo.

(iii) Serikali itahimiza uwekazaji katika tasnia ya mifugo.

(iv) Jitihada zitafanyika kuhimiza na kuwezesha uanzishaji wa vyama vya wafugaji vya fedha na mikopo.

# SURA YA NNE

## 4.0 MPANGO NA MFUMO WA UTEKELEZAJI WA SERA

### 4.1 Mfumo wa Utekelezaji

Utekelezaji wa Sera hii utazingatia mifumo na taratibu za kisheria na usimamizi wa viwango mbalimbali vya tasnia ya mifugo ambao utategemea sheria, kanuni na taratibu. Sera hii itatekelezwa kwa kuandaa mkakati na kutunga au kurekebisha sheria zilizopitwa na wakati.

### 4.2 Mfumo wa Kitaasisi

Malengo ya Sera ya Taifa ya Mifugo yatafanikishwa kutokana na ushiriki imara wa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Serikali, Sekta binafsi, Taasisi za elimu na vyama vya hiari. Sera hii inatambua umuhimu wa kuwepo kwa sera za sekta nyingine katika kufanikisha malengo yake. Utekelezaji wa sera hii utaoanishwa na ule wa sera za sekta nyingine pamoja na kuratibu kazi za wadau wengine katika kuendeleza tasnia ya mifugo nchini.

Utayarishaji wa sera hii unatoa fursa ya kuimarisha majukumu na kazi za Serikali Kuu ambayo ni sera, sheria, usimamizi na ufuatiliaji kulingana na mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji wa sekta ya umma. Serikali za Mitaa zimepewa majukumu ya kutayarisha na kutekeleza mipango ya maendeleo ambapo sekta binafsi inawajibika kutumia fursa na changamoto zilizopo.

Kulingana na Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa, Serikali hizi zitahusika kwa kiasi kikubwa kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo, mikakati na programu. Kutokana na mabadiliko ya majukumu ya Serikali, maafisa ugani wa mifugo wamehamishiwa katika Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi, utendaji na uwajibikaji. Serikali za mitaa zitaelekeza na kutekeleza mipango itakayowezesha kuendeleza juhudi za kusaidia kuendeleza uzalishaji mifugo.

### 4.3 Majukumu ya Wadau

#### 4.3.1 Wizara za Sekta ya Kilimo

Wizara za Sekta ya Kilimo zinajumuisha Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika; Maendeleo ya Mifugo; Viwanda, Biashara, na Masoko na Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kwa wakati huu, wizara hizi zinatekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS) na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP), ambazo ni nyenzo kuu ya Serikali Kuu za kuratibu na kufuatilia maendeleo ya Sekta ya Kilimo pamoja na kujumuisha maboresho yote yanayotokea nchini. Wizara ya Maendeleo ya Mifugo itasimamia utekelezaji wa

Sera ya Taifa ya Mifugo ambayo itatekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine.

### 4.3.2 Sekta ya Umma

Serikali pamoja na wadau wengine watahusika kutekeleza Sera ya Taifa ya Mifugo. Serikali itaharakisha mchakato wa mageuzi na kuendelea kuweka mazingira mazuri ya sera za uchumi za jumla yanayowezesha sekta binafsi kushiriki katika kukuza uchumi. Vilevile, Serikali itatoa huduma za kitaalam na endelevu zitakazohitajika kuongeza tija katika tasnia ya mifugo kwa lengo la kumwongezea kipato mfugaji na kuhakikisha uhakika wa chakula.

Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kutoa huduma muhimu za umma ambazo ni pamoja na ugani, taarifa, utafiti, mafunzo, miundombinu ya mifugo, kuandaa sera, udhibiti na kuzuia uharibifu wa mazingira. Aidha, serikali itahakikisha kuwa malengo na matarajio ya sera yanaainishwa kikamilifu katika muundo wa sera za uchumi.

#### (a) Wakala na Taasisi za Umma za Usimamizi na Udhibiti

Kuna wakala na taasisi mbali mbali za umma zinazojishughulisha na maendeleo ya Sekta ya Mifugo hususan, usimamizi na udhibiti. Wakala na taasisi hizo ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika nchi za Tropiki (TPRI), Baraza la Taifa la Kuhifadhi Mazingira (NEMC), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Ukaguzi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Tanzania (COASCO). Taasisi nyingine muhimu ni pamoja na Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), ambayo hudhibiti na kuendeleza sekta ya maziwa nchini na Baraza la Vetenari Tanzania (VCT) ambalo husimamia na kudhibiti maadili ya kazi za watoa huduma za mifugo.

#### (b) Taasisi za Mafunzo na Utafiti

Zipo taasisi za mafunzo na utafiti nchini kama vile Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Mzumbe (MU), Chuo Kikuu Huria (OUT), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Taasisi ya Utafiti wa Samaki (TAFIRI), Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika nchi za Tropiki (TPRI), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) ambazo hufanya tafiti na mafunzo kwa lengo la kutoa teknolojia muafaka ambazo zitatumiwa na wafugaji ili kuendeleza uzalishaji mifugo. Ushirikiano wa Wizara na taasisi hizo utaendelea kuimarishwa.

### 4.3.3 Sekta Binafsi

Serikali inatambua majukumu muhimu yanayotekelezwa na sekta binafsi. Sekta hii inajumuisha taasisi za fedha, wafugaji, wachungaji wahamaji, wakulima-wafugaji, wafanyabiashara ya mifugo, wasindikaji na wengineo. Sekta binafsi itahusika na shughuli za kibiashara za uzalishaji, usindikaji na masoko katika kuendeleza Tasnia ya Mifugo. Sekta binafsi inahitaji kuwekewa mazingira mazuri na Serikali ili iweze kushiriki kikamilifu na kufikia matarajio yaliyokusudiwa. Hapo baadaye, sekta binafsi inatarajiwa kuchukua baadhi ya majukumu muhimu ya Serikali ya kutoa huduma kama ugani, utafiti na mafunzo yatakayotoa fursa ya ajira.

#### (a) Vyama vya Wadau wa Mifugo

Vipo vyama mbalimbali vya wadau wa mifugo ikiwa ni pamoja na Chama cha Wasindikaji Maziwa Tanzania (TAMPA), Chama cha Wazalishaji wa Vyakula vya Mifugo Tanzania (TAFMA), Chama cha Wakulima Tanzania (TASO), Mtandao wa Wafugaji wa Mbuzi Tanzania (TAGONET), Mtandao wa Wafugaji na Uendelezaji wa Mbuzi Kanda ya Kusini Mashariki mwa Tanzania (SEGODEN), Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania (LAT), Chama cha Wafanyabiashara ya Mifugo na Nyama Tanzania (TALMETA) na Umoja wa Uendelezaji wa Uzalishaji wa Maziwa Tanzania (TAMPRODA).

Vyama hivi hutoa huduma mbalimbali kama mikopo, ugani, usambazaji wa pembejeo na upatikanaji wa masoko. Ushirikishwaji wa jamii na vyama vyao ni muhimu ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika kutekeleza sera hii, hivyo vitahimizwa kujiimarisha ili kuongeza tija. Kwa kuwa baadhi ya vyama hivyo bado ni vichanga, uwezeshaji wa kutosha unahitajika ili kuviwezesha kutumia teknolojia mpya.

#### (b) Asasi zisizo za Kiserikali na Asasi za Kijamii

Asasi zisizo za Kiserikali (NGOs) na Asasi za Kijamii (CBOs) hutoa mchango muhimu katika maendeleo ya sekta ya mifugo hasa katika utoaji wa utaalam, habari, uwezeshaji na kuweka pamoja raslimali katika ngazi za chini. Serikali itaweka mazingira mazuri kwa asasi hizo ili ziweze kutoa huduma ipasavyo. Ushirikiano imara na uratibu baina ya asasi hizo katika maendeleo ya jamii utahimizwa.

#### (c) Vyama vya Kitaaluma

Vyama vya Kitaaluma hutoa mchango muhimu katika maendeleo ya mifugo nchini. Kutokana na vyama hivi kujitegemea vinayo nafasi ya kutoa mawazo huru na kuchangia katika kuendeleza sekta ya mifugo, na pia kuweka uhusiano mzuri kati ya vyama hivi na serikali.

Baadhi ya vyama vya kitaaluma ni Chama cha Madaktari wa Mifugo Tanzania (TVA), Chama cha Wataalam wa Uzalishaji wa Mifugo Tanzania (TSAP), Chama cha Wachumi Kilimo Tanzania (AGREST) na Chama cha Viongozi Wanawake katika Kilimo na Mazingira Tanzania (TAWLAE) ambavyo hushiriki kuendeleza mifugo. Serikali itawezesha vyama hivi kwa kuvipatia mafunzo na ubadilishanaji habari na kuweka mtandao kati yao.

#### (d) Taasisi na Vikundi vingine

Vipo vyama vitatu muhimu vya wadau wengine wa mifugo, navyo ni Jumuiya ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Baraza la Kilimo na Mifugo Tanzania (TCAL) na Muungano wa wenye Viwanda Tanzania (CTI) na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA). Taasisi na vyama hivi huchangia katika kuendeleza Sekta ya Mifugo, na pia kuweka uhusiano mzuri kati ya wafugaji na serikali.

### 4.3.4 Washirika katika Maendeleo

Washirika katika Maendeleo wamekuwa wakitoa mchango mkubwa wa raslimali katika kuendeleza mifugo. Mchango huu ni wa kifedha, vifaa na kitaaluma katika kutekeleza mipango mbalimbali inayolenga kukuza uchumi. Hivyo, tutaendelea kushirikiana nao katika kuendeleza tasnia ya mifugo nchini. Baadhi ya washirika katika maendeleo ni Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (IFAD), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japani (JICA), SDC, GTZ, Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Uingereza (DFID), CFC, DANIDA, SIDA, NORAD, BADEA na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), Austria, Uholanzi na China.

## 4.4 Mfumo wa Uratibu

Mafanikio ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mifugo na ongezeko katika maendeleo ya tasnia ya Mifugo yanategemea kwa kiwango kikubwa uratibu wa wadau wote. Hii ni pamoja na uratibu wa Wizara zinazohusiana na Sekta nyinginezo za Kilimo, Taasisi, Washirika katika Maendeleo, Wakala na wadau wengine kama wafugaji na vyama vyao. Ili kuwezesha na kufanikisha uratibu baina na kati ya wadau, Serikali itaweka mkazo katika kuandaa na kuweka mfumo wa uratibu utakaohusisha wadau wote. Mfumo huo utatumia sheria na kanuni, mabaraza ya wadau, matokeo ya utafiti, huduma za kitaaluma, mfumo wa utoaji tahadhari za majanga, mabaraza ya wataalam na mfumo wa masoko ya mifugo.

Pia, ushirikiano na Taasisi za kikanda na kimatifa utaimarishwa. Taasisi hizo ni Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika (AU), Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Afya Duniani (WHO),

Shirika la Nguvu za Atomiki (IAEA) na Shirika la Kuimarisha Utafiti wa Kilimo katika Nchi za Mashariki na Kati mwa Afrika (ASARECA).

# SURA YA TANO

## 5.0 URATIBU NA USIMAMIZI WA SERA

Sera ya Taifa ya Mifugo ni mwongozo utakaotumika kufikia Dira na Dhamira ya Tasnia ya Mifugo. Lengo la muda mrefu ni kuwa na usalama wa chakula, kupunguza umaskini na kuongeza pato la Taifa kutokana na Sekta ya Mifugo. Ili madhumuni ya Sera hii yaweze kufikiwa, Wizara itaandaa mikakati na mpango wa utekelezaji.

Ufuatiliaji na usimamizi wa hatua kwa hatua ni muhimu katika utekelezaji na upimaji wa mafanikio ya sera. Jukumu la usimamizi na tathmini linabaki kuwa ni dhamana ya Wizara inayohusika na maendeleo ya mifugo. Hata hivyo, ufuatiliaji utategemea juhudi za pamoja na ushiriki wa karibu kati ya Taasisi za Umma, ikiwa ni pamoja na wizara zinazohusika na Fedha, Mipango, Kilimo, Biashara, Masoko, Ardhi na Serikali za Mitaa. Vilevile, ufuatiliaji wa uhakika utategemea juhudi za kuratibu na ushiriki wa karibu kati ya sekta za umma, binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na washirika katika maendeleo.